

ILE ISHARA

 . . . kuwa ni Neno. Kumbukeni kesho alasiri, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni kweli. Lakini mnajua mahali ninapomaanisha, ni kama maili hamsini upande wa juu wa barabara.

² Katika Kitabu cha Kutoka, tunasoma, usiku wa leo, kuanzia m—mlango wa 12 wa Kutoka, na kifungu cha 12 na kifungu cha 13. Ninaamini lingekuwa ni jambo zuri kama tungalisimama wakati tukisoma Neno, kwa kumheshimu Mungu. Kutoka 12:12

Maana nitapita kati ya nchi ya Misri usiku huo, nami nitawapiga wazaliwa wa kwanza wote katika nchi ya Misri, wa mwanadamu na wa mnyama; nami nitafanya hukumu juu ya miungu yote ya Misri; Mimi ndimi BWANA.

Na ile damu itakuwa ishara kweni katika zile nyumba mtakazokuwamo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lo lote likawaharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri.

³ Na tuinamishe vichwa vyetu.

⁴ Baba Mungu, tunaomba, usiku wa leo, ya kwamba tutajichunguza na tuone kama ile Damu imeninii vya kutosha, na inaonekana. Tunapozungumza juu ya Neno Lako, jalia Roho Mtakatifu atuongoze, katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

⁵ Somo letu la Maandiko, usiku wa leo, linaturudisha huko nyuma katika Kutoka. *Kutoka* ni “kuhama.” Na, hili, sisi sote tunajua wa—wakati huo, kwa ajili ya muktadha. Nitachukua somo la: *Ile Ishara*. Ishara, ishara ni nini? Ishara ni alama ya ninii. . . ya kwamba gharama imelipwa.

⁶ Kama vile kampuni ya reli, ama nauli ya basi. Wanapoendesha kampuni ya mabasi, unaingia, miji mingi ingali ina jambo hilo. Unaweza, ama tiketi ndiyo ishara. Kama ukienda kwenye kampuni ya reli, na, ama kampuni ya ndege, na kununua tiketi, si zile pesa unazotoa unaposafiri, ni ile ishara, tiketi yako, ama ishara yako ndogo uliyo nayo. Inaonyesha ya kwamba umelipia gharama inayotakiwa. Wanahitaji gharama fulani, na gharama hii imekwisha kulipwa.

⁷ Na somo tunalozungumzia, usiku wa leo, masharti ya Mungu kwa Israeli, masharti ya Yehova, yalikuwa ni damu ya mwana-kondoo. Hayo ndiyo yaliyokuwa matakwa yake, na yalikuwa yawe ndiyo ishara. Ile ishara ilionyesha ya kwamba masharti yalikuwa yametimizwa, ya kwamba kile Mungu alichohitaji kilikuwa kimetimizwa.

⁸ Kampuni ya reli inachohitaji, ishara inaonyesha takwa hilo limetimizwa. Nauli yako imelipwa. Uko tayari kuingia kwenye garimoshi, ndege, basi, chochote kile, bali unapaswa kuwa na ile ishara. Huwezi kuendelea bila ya ishara. Mengi ya makampuni hayatapokea pesa zako taslimu, unapoenda kwenye ndege, unakwenda pale, na kusema, “Ninataka kulipia tikiti yangu.” Nenda ukakate tiketi yako kwanza. Huna budi kuwa na hiyo tiketi, na ishara tu ndiyo unayopaswa kushika. Pesa, zenyewe, hazitafaa. Inakupasa uwe na ishara.

⁹ Uhai ulikuwa umetoka kwenye ile sadaka, na sasa ile damu ilikuwa ndiyo hiyo ishara. Maagizo Yake yalikuwa tayari yametekelezwa.

¹⁰ Hivyo ndivyo ilivyokuwa huko Misri, ule usiku wa kutisha, kabla tu mauti kupiga, lile pigo la mwisho. Mungu alikuwa ameonyesha ishara Zake kuu na maajabu huko Misri, uvumilivu na wema Wake, kwa Farao na watu wake wote. Alikuwa amepeleka ishara nyingi kubwa kote nchini. Aliwapelekea nabii, akawaonyesha ishara na maajabu, Nguzo ya Moto, na yote aliyokuwa amefanya. Na hata hivyo, yote aliyokuwa amefanya, hata hivyo hawakutubu. Hawakuja kwa Mungu. Walipuuza ishara Zake zote. Walimpuuza nabii Wake. Waliupuuza ule ujumbe. Walitaka kufanya walivyotaka wenyewe. Kwa hiyo Mungu alikuwa amechoshwa nao, kwa hiyo akasema, “Nitafanya utengano sasa kati ya wale wanaoamni na wale wasioamini.”

¹¹ Nafikiri tunaishi katika wakati ule sasa, ambapo Mungu anafanya uchaguzi. Watu wataamini ama hawataamini.

¹² Na Mungu alitaka ishara, na ishara hii ilikuwa ni mwana-kondoo asiye na hatia aliyekuwa amemweka badala ya kifo, katika bustani ya Edeni. Na sasa yule mwana-kondoo alipochinjwa, ile damu ilikuwa ipakwe kwenye mwimo na kwenye kizingiti, na ilikuwa ni ya kuonyesha ya kwamba masharti yalikuwa yametimizwa.

¹³ Loo, nafikiri hilo ni somo kuu kwetu tunapoliangalia. Kuona mwenye kuamini, akiabudu, kwa kuwa alikuwa ametambulishwa na ishara ya damu. Ilibidi atambulishwe, yaani mwaminio alipaswa amchukue mwana-kondoo, amchinje mwana-kondoo, mwana-kondoo mmoja kwa nyumba moja, achukue damu kwa hisopo, ambayo ni maskini kichaka kidogo kinachoota huko mashambani. Nayo, hayo majani ya kawaida, ndivyo tungeyaita, na ilibidi waipake hiyo damu. Inaonyesha, kwa kuipaka hiyo damu, kwa hisopo hii, hisopo inawakilisha imani. Mara nyingi, watu wanafikiri inawabidi kuwa na imani ya kimbinguni, ili wawe waamini. Sivyo. Ile hisopo inaonyesha hilo, ni majani tu ya kawaida ambayo mtu ungeweza kuyapata mahali popote, unayachukua, unayachovya kwenye damu, na kuipaka hiyo damu.

¹⁴ Ile damu, usiku wa leo, inapakwa kwa imani ya kawaida. Si kitu chochote cha kimbinguni; kiko papo hapo karibu yako, kila mahali. Kwa urahisi tu, kama vile tu mtoto, nyosha mkono na ukichukue, na upake hiyo Damu. Hisopo hiyo ni kama tu imani rahisi ya mtoto, kwa muumini. Si kitu usichoweza kukifikia. Haikulazimu kunyosha mkono mbali sana kuifikia.

¹⁵ Hisopo hii inayokua katika nchi ile, inaota kwenye nyufa za kuta, jani dogo mfano wa umbo la almasi. Unaweza kuliokota, mahali popote. Ni kama tu—kama tu vile nyasi ama magugu ambayo yangukuwa ma—ma—mashambani humu sasa; uyachukue tu, uipake, uiweke kwenye mlango.

¹⁶ Hivyo ndivyo imani inavyopaswa kutumiwa; chukua imani, hasa, na upake Damu ya Yesu Kristo, kwa imani, kwenye mlango wa moyo.

¹⁷ Hii ilikuwa iende kutenganisha na kutofautisha kati ya wale waliokuwa wakitoka Misri, na wale watakaokaa Misri, na kuangamia pamoja na Misri. Ilileta tofauti.

¹⁸ Ni ajabu, jinsi ambayo Mungu daima hutenda kazi kwa miujiza, vionyo, ishara, na kadhalika. Daima Yeye amefanya jambo hilo. Hiyo ndiyo njia Yake ya kufanya jambo lolote. Yeye kamwe hafanyi jambo nje ya hizo. Mungu hatendi neno kamwe mpaka amelifanya kwa jinsi hiyo.

¹⁹ Jinsi ambavyo Mungu huanza, hivyo ndivyo Mungu anavyomalizia. Yeye hana mpaka, ni mwenye nguvu zote, yupo mahali pote, anajua yote. Hahitaji msaada wa mtu yeyote. Hahitaji ufasiri wetu, kama nilivyosema jana usiku. Yeye hahitaji sisi kulifasiri Neno na kusema kile linachomaanisha. Yeye hunena kile linachosema litafanya, huo ndio ufafanuzi wake. Hakuna mtu anayepaswa kulifafanua. Mungu anaposema, “Na iwe,” na ikawa, huo ndio ufafanuzi Wake wa Hilo.

²⁰ Huenda tukasema, “Siku za miujiza zimekwisha. Hakuna kitu kama ubatizo wa Roho Mtakatifu.” Mtu anayeuamini, Mungu hunena naye, na huo ndio ufafanuzi. Wanao! Hiyo, wao wanajua kwamba wanao, kwa kuwa Mungu hutoa ufafanuzi Wake Mwenyewe kwa Neno Lake.

²¹ Hilo ndilo alilokuwa akitaka usiku ule, kutenganisha waamini na wasioamini. Mwamini, mwabudu, alitambulishwa na sadaka yake. Hana budi kupaka damu. Halikuwa jambo la “Mchukue mwana-kondoo na umchinje, uweke hiyo damu huko nje mahali fulani, ama uiweke kwenye sinia, ama uichukue uipeleke kwa majirani.” Ilimbidi kupaka hiyo damu!

²² Hivyo ndivyo ilivyo, usiku wa leo. Tungeweza kuja na kukubaliana na kila kitu Mungu anachofanya, hilo silo analotaka. Unapaswa kupaka. Haitoshi mpaka utakapoipaka. Damu haina budi kupakwa, hiyo inaonyesha ya kwamba umetambulishwa. Mwabuduo aliweka mkono wake juu ya

mwana-kondoo, na kisha akamchinja, akajitambulisha na ile sadaka.

²³ Ni jambo lilo hilo tunalofanya, usiku wa leo, ni kuweka mkono wetu juu ya Sadaka yetu, na kujitambulisha pamoja na Yeye. Naye ni Neno. Inatupasa kutambulishwa kupitia kwa Kristo tu, ndipo tunapotambulishwa na Neno, kwa sababu Yeye ni Neno, amekuwa Hilo daima. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele!”

²⁴ Kiasi fulani cha Neno kimewekewa kila kizazi. Mungu humtuma mtu fulani katika wakati huo naye hulitambulisha Neno hilo, kwa kujifasiria Mwenyewe.

²⁵ Kanuni za imani na kadhalika daima zimeingiza kanisa katika machafuko makuu, kila mtu alisema, “Vema, njia ndiyo *hii*, na *hii* ndiyo njia, na *hili* ndilo linalokupasa kufanya.” Bali Mungu huingia, na huingia jukwaani na kufanya alilosema kutimia, hiyo ndiyo fasiri yake. Haihitaji mtu yeyote kulielezea; si mtu mwenye dhambi, wala mashirika, wala madhehebu yoyote makubwa, wala kitu chochote kile, kufasiri Neno; askofu fulani, askofu mkuu, papa, wala chochote kile. Siyo hivyo. Mungu hujifasiria Mwenyewe. Wakati Yeye alipoliahidi, Yeye hulitimiza.

²⁶ Kama vile nimesema, mara nyingi. Yeye aliposema, “Iwe Nuru,” na nuru ikawepo, hiyo ndiyo fasiri yake. Haihitaji tena, kitu chochote zaidi kujaribu kulifasiri. Mungu hulifasiri, Lenyewe.

²⁷ Damu hii ikipakwa, na mwabudu aliyetambulishwa alijitambulisha na damu hiyo, kwa kuipaka katika nyumba yake mwenyewe, kwenye mlango, ambapo asingeweza kutoka wala kuingia bila kutambuliwa na damu. Mfano mkamilifu sana, wa leo hii, wa Damu ya Yesu Kristo. Basi, hiyo damu ilikuwa ni ishara ya utambulisho. Kristo ndiye ishara ya utambulisho wa mwaminio leo.

²⁸ Uhai wa mnyama. Siku zile, ilikuwa ndio sababu wao kupaka damu ya kawaida, kuichukua kwa hisopo, kuiweka juu ya mhimili na kizingiti, ni kwa sababu mnyama huyo... Mwabuduo anayeweka mikono yake na alijitambulisha na mnyama huyo, uhai ule uliokuwa katika mnyama usingeweza kurudi juu ya mwabuduo, kwa maana mnyama hana nafsi. Yeye hajiendelezi hata kidogo.

²⁹ Tunaona, leo, ya kwamba sisi wanadamu, ingawa tumeanguka, katika hali hii ya kuanguka, tunajenga nyumba zetu zilizo bora zaidi, tulitengeneza, tunatengeneza gari bora zadi. Tunachukua kile Mungu ameumba, tunakipotosha, na kukifanya kitu cha kujisaidia sisi wenyewe. Inaonyesha ya kwamba sisi ni wana wa Mungu, katika hali yetu ya kuanguka,

hata hivyo tuna nafsi. Hatuwezi kuumba, kama Mungu alivyofanya. Bali tunaweza kuchukua kile alichoumba, na kufanya kiumbe kama hicho kutokana na kile Yeye amekwisha kuumba tayari.

³⁰ Mnyama hafanyi hivyo. Mbwa angali anaishi jinsi ile ile alivyoishi. Ndege angali anajenga kiota. Na samaki ana mahali pake pa kutagia mayai. Hakuna tofauti pale, kwa sababu (gani?) wao hawaninii. . .hawana nafsi. Lakini, inathibitisha ya kwamba mwanadamu yuko katika mfano wa muumba wake. Kwa hiyo, kwamba wakati mnyama alipokufa na damu yake ilitoka, seli ilipasuliwa, uhai umo katika chembe ya damu. Na chembe ya damu ilipopasuliwa, damu hiyo ikawa imetoka, ilimbidi mwabuduo kuchukua damu yenyewe na kupaka kwenye mlango, kusudi ipate kuonekana kwa jicho la kawaida. Kwa sababu, ule uhai uliokuwa ndani ya mnyama usingeweza kumrudia mtu huyo, kwa kuwa hakuwa na nafsi, kwa hiyo isingeweza kuchanganyikana na nafsi ya mwanadamu. Uhai wa mnyama hautamrudia mwanadamu.

³¹ Sasa, Sadaka yetu leo, sio mwanadamu tu wa kawaida, bali ilikuwa ni Mungu Mwenyewe aliyetambulishwa katika mwili hapa duniani. Wakati seli hiyo ya Damu ilipopasuliwa, si kwamba tu nafsi ya Mwanadamu, ama roho ya Mwanadamu; bali Mungu Mwenyewe, Ambaye alitambulishwa katika Mtu yule, inamrudia mwaminio, katika ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo Ishara ambayo Mungu anataka leo. Ishara ya leo, inayotupasa kuwa nayo, haina budi kuwa ni Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo ishara inayotakiwa na Mungu. Tutawathibitishia hilo kwa Maandiko.

³² Bila ya Roho Mtakatifu, huonyeshi Ishara. Huyu ndiye ile Ishara, inaonyesha ya kwamba . . .ya kwamba umejitambulisha mwenyewe na ile Sadaka, na Mungu amekurudishia hiyo Ishara, kuonyesha ya kwamba umekubalika tayari. Mpaka jambo hilo litakapofanyika, haidhuru wewe ni mzuri jinsi gani, unajua kiasi gani, jinsi ulivyo profesa wa chuoni, mtu mzuri, mhubiri, chochote kile. Hutambuliwi hata kidogo mpaka unapoweza kuonyesha ile Ishara.

³³ Israel; katika kule kutoka, walipotoka wakati ule, ilibidi wawe na ile ishara, kuthibitisha ya kwamba walitambulishwa na sadaka yao.

³⁴ Na, usiku wa leo, Mungu anataka Ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa thibitisho ya kwamba tumetambulishwa katika ufufuo wa Yesu Kristo. Hakuna kitu kilichopunguka kwake. Biblia inafundisha jambo hilo, dhahiri, nasi hatuna budi kuliadini. Ni Neno la Mungu. Mungu analitaka hilo. Tuna kutoka, tena. Sote tunajua jambo hilo. Israeli walikuwa wakienda kwenye nchi ya ahadi, vivyo hivyo Bibi-arusi atakwenda Nyumbani kwake, hivi karibuni sana.

35 Sasa tunaona, ile damu ilikuwa ni ishara, na—na ilitambulishwa. Kila mtu alitambulishwa kwa damu.

36 Roho Mtakatifu ndiye Ishara yetu, leo, ya kututambulisha, pamoja na Yesu Kristo, katika kufufuka Kwake. Damu inapakwa kwa imani.

37 Ile damu yenyewe isingeweza kuunyunyiza kila moyo, tunajua hilo, kwa sababu ilimwagwa pale Kalvari. Iliowesha ardhi. Lakini kutoka, wakati hiyo seli ya Damu ilipopasuliwa, ilimfungulia Mungu, kupitia nguvu za utakaso ambazo hiyo Damu ilikuwa nazo, za kuwarudia waaminio.

38 Mungu, hapo mwanzo, alikuwa ni Mungu, Baba, ambaye aliishi juu ya wote.

39 Ni kama tu vile ile—ile Nguzo ya Moto ilivyowaongoza wana wa Israeli kupitia jangwani, Yeye alishuka juu ya ule mlima. Kama mtu yeyote aliugusa huo mlima, kwa sababu, hana budi kuuawa. Mungu ni mtakatifu, wala hawezi kuvumilia dhambi kwa namna yoyote. Na mtu aliyeugusa huo mlima alikufa, hata mnyama ilibidi achomwe kwa upanga. Wakati Mungu aliposhuka, alikuwa mtakatifu.

40 Ndipo Mungu, akijishusha, alishuka na akafanywa kwa umbo la Mwanadamu, tupate “kumshika, kumgusa,” Biblia ilisema. Katika chembe ile ndogo mno ya Damu!

41 Wayahudi wengi wanataka kusema Yeye alikuwa Myahudi. Wengi wetu tunataka kusema Yeye alikuwa ni Myahudi. Yeye hakuwa Myahudi wala Mmataifa. Alikuwa Mungu. Yeye alikuwa muumbaji Aliye Hai, kwa mkono wa mwenyezi Mungu. Aliumba maskani alimoishi, ambayo tunajua kama Mwana wa Mungu. Hiyo ni kweli. Ule uungu, uungu mkuu wa Yesu Kristo, maana Mungu aliishi ndani Yake.

42 Petro alisema, “Enyi waume wa Israeli; Yesu wa Nazareti, Mtu aliyedhihirshwa na Mungu, kwa ishara na maajabu, mmemchukua kwa mikono ya watu wabaya na kumsulubisha. Sisi tulikuwa mashahidi wa kufufuka Kwake,” wakati Roho Mtakatifu alipokuwa amekwisha kumwagwa juu yao.

43 Sasa tunaona ya kwamba, ya kwamba katika jambo hili kuu, ya kwamba, Mungu alipokuwa akijitambulisha na Israeli huko nyuma, na akitaka utambulisho huo.

44 Sasa tunaona hapa, Wayahudi wangaliweza kusema, huenda wangesema, “Vema, sasa, hebu ngoja kidogo. Mimi ni ninii . . . Mimi ni Myahudi. Mimi—mimi niko katika agano la Ibrahimu. Nimetahiriwa.” Lile agano lilikuwa, lilibatilika, kama ile ishara haikuonyeshwa. Wazia jambo hilo! Ninazungumza juu ya Ishara ya siku hii. Kama hiyo damu haikuwa imeonyeshwa, ishara hiyo, sijali ni kiasi gani ungeweza kuonyesha ya kwamba wewe ulikuwa u Myahudi, kwamba ulisema uliamini kiasi gani. Huenda ulikuwa rabi, kasisi, ama chochote kile, hata hivyo ile

ishara ilipaswa kupakwa. Hakuna kuingia na kutoka, ndio au siyo; mpaka alipoiona ile damu, Yeye angepita juu yao.

⁴⁵ Jamaa fulani wanaweza kusema, “Njoo huku kando. Ninaweza kuthibitisha ya kwamba nilitahiriwa kwenye siku ya nane. Kuhani ana kumbukumbu la hili. Jina langu liko kule kwenye kitabu.” Hilo halikuwa na uhusiano wowote nalo. Ishara—ishara ilikuwa ninii. . . Kama ishara haikuwekwa, lile agano lilibatilika. Halikuwa na nguvu.

⁴⁶ Inatupasa kukumbuka vile Mungu alivyosema. Yeye kamwe haghairi, bali huyaongezea. “Watu wa kale, mnawasikia wakisema, ‘Usizini,’ lakini nawaambia, ya kwamba kila mtu amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye tayari.” Yeye haghairi; huliongezea. Yeye hukuza. Hivyo ndivyo anavyofanya. Kazi Zake zote, Yeye daima huzikuza.

⁴⁷ Hapo ndipo tunapotembea kutoka kwenye wakati mmoja wa kanisa, kutoka kwa Luther, kuingia kwa Wesley, kuingia katika Pentekoste, na kuendelea na kuendelea tunaposonga mbele. Tunapozidi kupiga hatua kwenda juu, Mungu anaendelea kulikuza Neno lile lile, analifanya kuendelea tu namna hiyo, mpaka hatimaye kanisa litafikia kwenye sura ya Yesu Kristo, ambalo litakuwa ndio Bibi-arusi Wake ambaye Yeye atamchukua ampeleke Nyumbani, kabisa, jambo tunalolitazamia leo. Hakika, tunatambua ya kwamba kanisa litapitia kwenye ile dhiki, bali Bibi-arusi hatapitia. Atatolewa kwenye kanisa, kama tu—kama tu vile Israeli walivyotolewa Misri. Tunaona sasa ya kwamba Roho Mtakatifu alikuwa ndiye sasa anayetutambulisha pamoja na Yesu Kristo.

⁴⁸ Huenda Wayahudi wangesema, “Naam, sisi ni Wayahudi wa agano.” Lakini kama hawakuwa na ile Ishara, agano hilo lilikuwa ni bure.

⁴⁹ Ni jambo lile lile leo. Haidhuru sisi ni wazuri jinsi gani, haidhuru. . . Huenda ukasema, “Vema, mimi ni. . . Nimefanya jambo *hili*, na nimefanya mambo haya yote. Na nimelipa fungu langu la kumi. Nimekuwa mfuasi wa kanisa, nami ninafanya *haya* yote.” Mungu anahitaji ile Ishara, kuonyesha ya kwamba umetambulishwa pamoja na Sadaka yako, Ile unayodai unayo, Ile unayoamini ya kwamba unayo.

⁵⁰ Petro alisema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

⁵¹ Ni nani mtu huyo mwenye dhambi atakayebadilisha Hilo, na kusema, “Siku za miujiza zimekwisha”? Ni nani atakayefanya jambo hilo, na kusema ya kwamba Neno la Mungu lilikosea?

⁵² Wakati Yeye aliposema, “Kila atakayeliita Jina la Bwana! Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu,

na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.” Atawapiga muhuri wa ile Ishara.

⁵³ Hiyo inaleta tofauti kati ya muumini na asiyeamini. Kulikuwako na wale waliotiwa muhuri na ufalme wa Mungu, na wale waliotiwa alama kwa alama ya mnyama, na wale waliotiwa alama na alama kwa mnyama wasingeweza kuchukua Muhuri wa Mungu. Jambo lile lile linaingia leo, nasi tunalionga moja kwa moja mbele ya macho yetu wenyewe.

⁵⁴ Haidhuru wewe ni mzuri jinsi gani, unavyosema kiasi gani wewe ni muumini, Mungu anataka ile Ishara. Aliitaka huko Misri. Anaitaka usiku wa leo. Anaitaka usiku wa leo. Hata hivyo, Ishara inatakiwa tu vilevile katika wakati huu kama ilivyotakiwa katika wakati huo. Sijali kama ulikuwa mwanafunzi wa Biblia, jinsi unavyoweza kuelezea Maandiko vizuri; Shetani anaweza kufanya jambo lile lile. Lakini, kumbuka, hilo halina uhusiano wowote nalo. Mungu anahitaji jambo moja, hilo ni ile Ishara. Ishara inaonyesha ya kwamba wewe umetambulishwa pamoja na Sadaka yako unayodai ya kwamba unaiaibudu. Amina. Jambo ndilo hilo.

“Nitakapoiona ile damu,” ama ile ishara, “hiyo damu itakuwa ni ishara; na nikiiona hiyo damu, nitapita juu yenu.”

⁵⁵ Kifo kilikuwa tayari kuipiga Misri wakati huo, wakati wowote. Ulikuwa ni wakati mkuu, wa ajabu sana. Mungu alikuwa amewaonyesha neema, kwa kuonyesha nguvu Zake, ishara. Hata hivyo hawakutamani kutubu, wala kurudi. Hawakutaka kitu kama hicho. Hawakuamini hilo. Hawakuamini ujumbe uliokuwa ukiendelea. Mungu alikuwa amewatumia ujumbe; hawakuuamini. Wangali walitaka kuendelea moja kwa moja jinsi walivyokuwa wakiendelea.

⁵⁶ Ni mfano halisi tu wa siku hizi, jambo lile lile. Kila tukio la kiroho na kila ishara ya kiroho ni onyo kutoka kwa Mungu, ya kwamba jambo fulani liko karibu kutimia, kama ishara hiyo inatoka kwa Mungu. Kama imebuniwa na mwanadamu, ha—haifai kitu. Bali kama imetumwa na Mungu! Mtu yeyote anajua, kila mtu anajua, ya kwamba Mungu hutuma ishara, kama ni ishara ya mbinguni, Yeye hutuma Ujumbe pamoja na ishara hiyo. Daima hufanya hivyo, Yeye kamwe hashindwi kufanya jambo hilo. Tukiona mambo ambayo si ishara za Mungu, vema, basi hazitakuwa chochote, maana Mungu hahusiki. Lakini wakati Mungu anahusika na jambo hilo, Ujumbe utaifuata hiyo, na Ujumbe huo hauna budi kuwa umetoka kwenye Maandiko. Huo hauna budi kuwa ni Ujumbe wa Kimaandiko. Hauna budi kuja BWANA ASEMA HIVI. Kila tukio la kiroho ni ishara kutoka kwa Mungu.

⁵⁷ Kama vile Ujumbe na ishara zinazofuata, katika siku hii, kama ilivyokuwa katika siku za hizo siku nyingine tulizopitia, katika wakati wa Biblia. Wala hakuna wakati mwingine hili

lingalitukia mpaka sasa. Hakuna wakati mwingine Ujumbe huu ungaliweza kuja mpaka sasa. Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.” Ujumbe huo haungekuwako mpaka sasa. Ulimwengu haukuwa katika hali hiyo kama ulivyokuja kufikia sasa. Hii ndiyo saa ambayo Yesu angeweza kutokea wakati wowote.

⁵⁸ Wanawali waliolala wakiingia, wakijaribu kununua Mafuta. Huo ndio wakati ule ambapo Bibi-arusi aliingia, na hao wengine waliachwa hapa. Je! uliwahi kuwazia yaliyotukia? Waliendelea moja kwa moja wakihubiri na wakifikiri walikuwa wakiokoa nafsi, na kila kitu, wala hawakujua jambo hilo. Hawakujua kitu juu ya jambo hilo. Kanisa litaendelea, likifikiria nafsi zinaokolewa, na chochote kile, na Kanisa tayari (Bibi-arusi) ametiwa muhuri. Halijui! Hakika. Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema hasa. Nuhu aliingia katika safina, na Mungu akaitia muhuri. Hakika. Na wakati unakuja ambapo wanaume na wanawake watamlilia Mungu, na hata wafikiri wamepata kitu fulani, wakati hawajapata. Hiyo ni kweli kabisa. Maandiko yanasema jambo hilo.

⁵⁹ Vivyo hivyo, inatupasa kukumbuka ya kwamba Mungu ni “mvumilivu, maana hapendi mtu yeyote apotee.” Yeye daima hutuma ishara Zake, maajabu Yake. Na halafu anapokuwa yuko tayari kufanya jambo lolote, yeye humtenganisha muumini na asiyeamini.

⁶⁰ Angalieni, basi, jinsi Yeye anavyowaandalia watu Wake wa nchi ya ahadi. Angalia vile alivyowafanyia watu wake wa nchi ya ahadi pale, apate kuhakikisha ya kwamba hawatachanganyikiwa katika namna fulani ya itikadi. Yeye alifanya nini? Aliwatumia nabii, Musa, akiwa na ujumbe, akilitambulisha Neno la Mungu. Na, kumtambulisha Musa, Yeye alituma Nguzo ya Moto iliyoning’inia juu yake. Amina. Kisha, ili kuwapa hakikisho kamilifu, Yeye alihitaji ishara. Amina. Huyu hapo mjumbe, ujumbe, na thibitisho, na ile ishara, hakikisho kamilifu ya kwamba hawakuwa na kitu cha kuhofia. Haidhuru ni mapigo mangapi yapige, yale kila mtu asemayo, wao wametiwa muhuri.

⁶¹ Israeli wakitoka Misri, kama nilivyosema dakika chache zilizopita, ni mfano wa Bibi-arusi akitoka kanisani. Wakati Musa alipoanza huduma yake, Israeli walikusanyika mahali pamoja, katika Gosheni, wakaanza kuomba; kwa kuwa walijua ya kwamba wakati ulikuwa umewadia, kwa kuwa walijua ya kwamba kitu fulani kilikuwapo. Yule mkombozi alikuwa tayari amekuja. Mungu alikuwa akifanya kazi, akifanya mambo, akionyesha kile alichokuwa anataka kwenda kufanya. Walikuja toka sehemu zote za Misri, kama tu watakavyofanya katika ile Siku ya Kuja Kwake. Watawatoa watu kutoka katika Methodisti, Baptisti, Lutheri. Wote wale ambao wametambulishwa katika

Kristo, kwa ile Ishara, Mungu atawanyakua pamoja Naye wakati atakapokuja.

⁶² Tunasoma hapa katika Waebrania, mlango wa 10, kifungu cha 26, “Kama tukifanya dhambi kusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile Kweli, haibaki tena Dhabihu kwa ajili ya dhambi, bali kuna kuitazamia hukumu za kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kumla yeye apingaye.” Hiyo ni kusema, kama tusipoamini makusudi baada ya sisi kuwa na ujuzi wa ile Kweli, hakuna tena Dhabihu kwa ajili ya dhambi.” Wazia jambo hilo! Haidhuru unawazia nini moyoni mwako, ile Ishara haiwezi kupakwa; kama ukiikataa Hiyo mara ya mwisho, ndipo haiwezi kupakwa. “Yeye, kwake yeye anayetenda dhambi ama kutokuamini kusudi.”

⁶³ Tunapona zile ishara kubwa za mwisho, na nyakati zikija, jinsi tulivyo sasa na ahadi ya Neno! Kila Neno ambalo tumeahidiwa kabla ya wakati wa mwisho, tuko kabisa katika hili hivi sasa. Hata kwenye kule kutiwa alama ya mnyama, na madhehebu kuungana pamoja, na—na utawala wa papa kuingia, na kila kitu jinsi kilivyo hasa. Ulimwengu unaning’inia huko ng’ambo, makombora ya atomiki yako kwenye vibanda vyake. Na Mungu anazungumza kupitia watumishi Wake, makanisani, na kuwatoa nje, na kuonyesha ishara ambazo aliahidi angezifanya kabla tu ya kule Kuja Kwake. Tuko katika wakati wa mwisho. Ishara inatakiwa. Naam, bwana. Sasa tunajua ya kwamba mambo hayo ni kweli. Nayo yalikuwa, yalikuwa ni mfano tu wa yale tunayopitia sasa. Tunapona ishara hizi kuu zikija wakati wa mwisho, zikituonya, wakati umewadia.

⁶⁴ Usitende dhambi makusudi. Usiasi makusudi. Kama kuna jambo fulani ndani yako, linalosema, “Vema, sasa, sioni ambapo ninahitaji Roho Mtakatifu. Huenda nisimhitaji. Ninaamini, nilipoamni, nilimpata.”

⁶⁵ Paulo aliwaambia, watu waliomwuliza swali hilo, alisema, “Je! mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?”

⁶⁶ Roho Mtakatifu ndiye ile Ishara. Mtu humwamini Mungu, hiyo ni kweli vya kutosha. Bali Roho Mtakatifu ni karama ya Mungu, ni kitu tofauti na imani yako. Imani yako ndiyo inayokitumia, hiyo ni kweli kabisa, bali Roho Mtakatifu ni shahidi. Tutaona, katika dakika chache tu, jinsi anavyotenda kazi, na nini kinachotukia, ambapo tunaweza kuwa na uhakika, ambapo ambapo tunajua mahali tuko sawa, ama hatuko. Anatuonya ya kwamba wakati umewadia.

⁶⁷ Inatupasa kupendana. Katika wakati huu, kanisa na muumini wanapaswa wawe kitu kimoja. Waumini, waumini wanapaswa kujitenga na mambo yote ya ulimwengu. Kila kitu kisicho cha kumcha Mungu, muumini anapaswa kujitenga nacho.

⁶⁸ Angalia, haikuwabidi tu kuja pamoja na kuzungumza juu ya jambo hilo, na kusema, “Tunaliamini.” Walipaswa kuja pamoja na kupaka damu. Sio kuja, kusema, “Loo, hakika, ninaamini Hilo,” na kuenda nyumbani. Iliwapasa kuja na kupaka damu, kusudi ile ishara iweze kuonekana; waingie chini yake.

⁶⁹ Hiyo ni leo. Tunaketi na kusikia Ujumbe ukihubiriwa. Tunausoma kutoka katika Biblia. Tunasema, “Loo, naam, ninaamini Hayo.” Hilo silo Mungu analotaka. Haidhuru unauamini kiasi gani, inakupasa uwe Nao. Kanisa, amka!

⁷⁰ Marekani, hii ndiyo saa yenu ya mwisho! Hukumu iko kwenye mizani, huko juu, kwa taifa hili. Kama Mungu angeliacha taifa hili likwepe yale limefanya sasa, Yeye angewajibika kuiinua Sodoma na Gomora, na kuomba msamaha kwa kuiangamiza. Hiyo ni kweli. Tunalipia dhambi zetu. Tunafanya jambo lile lile walilofanya huko Sodoma.

⁷¹ Na Mungu ametuma Ujumbe vile vile hasa alivyofanya huko Sodoma. Vivyo hivyo hasa. Aliutuma mmoja kwa kanisa kule nje pamoja na kundi la Lutu; na huko Sodoma; na akautuma kwa Wateule, na kadhalika. Na akauthibitisha, ya kwamba kanisa limekaa katika hali lililokuwamo katika siku za—za Lutu, kama vile Yesu alivyosema ingekuwa tena. Enyi marafiki, limo mikononi mwetu, tutafanya nini nalo?

Unasema, “Ati damu imo mikononi mwenu?” Naam.

⁷² Unafikiri Oswald aliwazia nini wakati alipokuwa ameketi katika chumba kile, hivi majuzi, kwa kumwaga damu ya binadamu mwenzake, kumpiga risasi Rais katika mauaji ya kisiasa? Naye alikuwa ameketi pale, akijua ilimbidi kukabiliana na mahakama ya jamhuri, wakati Mahakama hiyo Kuu ingemtazama, kwa macho yenye hasira, yakijua ya kwamba mikononi mwake mlikuwamo na damu ya Rais wa Marekani. Alikuwa kwenye kizimba cha kutokwa na jasho.

⁷³ Inapaswa kumfanyiaje mtu, wakati unajua umeikanyaga Damu ya Yesu Kristo, na umekataa kukubali jambo hilo? Unaketi kwenye kizimba cha kutokwa na jasho. Si kwamba tu utahukumiwa na Mahakama Kuu; na Mungu mwenye hasira ambaye anaweza kuutupilia mbali mwili, na kuitupa nafsi katika kuzimu. Simama! Angalia! Sikiliza! Kubali! Tunamkanyaga tu, kwa urahisi, na tunafikiri Yeye anapenda watu sana.

⁷⁴ Kijana mwanamume alisema, hivi majuzi, “Mungu ananipenda sana!”

⁷⁵ Mungu ni Mungu mwema, hiyo ni kweli, bali Yeye ni Mungu mwenye hasira, pia. Yeye ni Mungu wa hukumu. Yeye ni Mungu wa hasira. Tunashindwa kushika jambo hilo. Mnamfanya mwema sana mpaka mnamfanya maskini babu punguani. Yeye si babu punguani. Yeye ni mwenyezi Mungu, wala hana wajukuu. Ana wana na binti za Mungu, si walioingizwa kwa kupewa

mikono na kufanywa wana. Huna budi kuzaliwa mara ya pili, na Damu ipakwe! Ni wana na binti za Mungu. Si maskini babu mzee mpole, anayewaachilia watoto Wake, wajukuu kufanya chochote wanachotaka. Yeye si babu. Yeye ni Baba. Naam, bwana. Kila mtoto hana budi kuzaliwa Naye. Yeye ni baba wa kurekebisha.

⁷⁶ Tunajua ya kwamba saa hii iko hapa, na hukumu imekaribia. Tutafanya nini na jambo hilo? Ningechukia kuwa na Damu Yake juu yangu. Kuna njia moja tu ambayo ungaliweza kuiondoa kwako.

⁷⁷ Huwezi kuiosha itoke. Pilato alijaribu jambo hilo. Alijaribu kukwepa wajibu wake kwa kumpelekea mtu mwingine, na kusema, “Mpelekeni kwa Kaisari fulani, ama mtu mwingine kama huyo, na mwone vile atakavyofanya.” Ikawa ni kinyume cha matarajio. Likamrudia moja kwa moja. Kweli!

⁷⁸ Na, leo, tunajaribu kusema, “Ningefanya hivyo, kama mume wangu! Naam, Ningefanya hivyo, kama mke wangu! Ningefanya hivyo, kama kanisa langu!” Inakuwa ni kinyume cha matarajio, linakurudia moja kwa moja. Unaposema, “Loo, vema, kanisa langu linaamini jambo hili.” Lakini wakati Yesu Kristo anaposhuka akaja kwenye mikutano hii na kujitambulisha katika Maandiko, ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele; sijali jinsi fasiri yako ilivyo, linakurudia moja kwa moja, na liko mikononi mwako. Hakuna kitu, ndugu na dada, mnachoweza kufanya.

⁷⁹ Enyi marafiki, kumbukeni jambo hili, ninyi mlio leo huko California, mko mwishoni mwa Pwani ya Magharibi hapa. Na ustaarabu umesafiri pamoja nalo, na kila kabwela anaingia. Na, halafu, litaenda Israeli wakati Kanisa litakaponyakuliwa. Tahadharini! Kuna njia moja tu ambayo unaweza kuiondoa Damu ya Yesu mikononi mwako, ni kuitia ndani ya moyo wako. Ipo njia moja tu. Haitafanikiwa kwa njia nyingine yoyote. Kasema, “Nitakapoiona ile Damu, wakati imetiwa mahali sahihi!”

“Vema,” unasema, “ninaiamini ile Damu.”

⁸⁰ Vipi kama walikuwa wameitupa huko nje nyuma uani? Vipi kama walikuwa wameiweka kwenye nyumba ya kuku? Vipi kama walikuwa wameitupa kwenye gereji? La. Ilipaswa kutiwa mahali fulani pamoja, hapa palikuwa ni kwenye kizingiti.

⁸¹ Moyoni, hapo ndipo Mungu anapoitaka ile Damu, leo. Si mikononi mwako, bali moyoni mwako, Mungu anaitaka.

⁸² Na iko mikononi mwako, leo. Kama hujamkubali, na una Muhuri moyoni mwako, iko mikononi mwako. Utambulisho Wake wa Maandiko Yake, katika siku hizi za mwisho, unaiweka moja kwa moja mikononi mwako. Tunaweza kufanya nini na huyu Yesu aitwaye Kristo? Tutafanya nini Nayo? Jambo moja tu,

ni kuionyesha wazi Damu Yake, kwa kuiacha iwe moyoni mwetu, kwa Roho Mtakatifu.

⁸³ Sisi, tunawajibika. Yeyote wetu asiye chini ya Damu hiyo, Mungu hawajibiki kwa jambo hilo, hata kidogo.

⁸⁴ Ilibidi familia yote ije, si mshiriki mmoja tu. Aseme, “Vema, kama baba ni mtu mzuri, yeye ni mhubiri, nitaokolewa.” La, bwana. Baba yako na mama yako wacha Mungu hawana uhusiano wowote na wewe. Wewe ni mtu binafsi.

⁸⁵ “Mimi ni mfuasi wa lile kanisa takatifu, kanisa *lile*.” Kanisa halina uhusiano wowote na Wewe.

⁸⁶ Hakuna kitu kama kanisa takatifu. Hakuna kitu kama mtu mtakatifu. Kuna Roho Mtakatifu aliye pamoja na watu. Roho Mtakatifu kanisani. Hakuna milima mitakatifu, hakuna mahali patakatifu; ni Mungu mtakatifu. Si wewe ukiwa mtakatifu, mimi nikiwa mtakatifu; Yeye ndiye aliye mtakatifu.

⁸⁷ Tunawajibika Kwake, si kwa kanisa. Tunawajibika kwa Mungu na kwa Neno Lake, naye Mungu ni Neno. Biblia ilisema alikuwa. Tunawajibika kwa jambo Hilo. Huyu ni Yesu Kristo.

⁸⁸ Angalia yale aliyotenda wakati huo. Tunaona ya kwamba familia yote ilikuwa salama tu wakati ile ishara ilipoonyeshwa wazi. Wakati ishara ilipoonyeshwa wazi, walikuwa salama.

⁸⁹ Angalia katika mlango wa pili wa Yoshua, uone hapa ya kwamba kahaba aliyeamini, jina lake Rahabu, Mmataifa malaya, huko ng'ambo ya mto, walipoingia kwenye nchi ya ahadi, wapelelezi walienda kule kupeleleza. Familia yake yote iliokolewa chini ya ile ishara, hiyo peke yake. Kumbukeni, Malaika wa kuangamiza wa Mungu aliitakabali ishara hiyo. Wakati makanisa yalipoangamia, meya alipoangamia, mji huo ulipoangamia, mfalme alipoangamia, liwali, wenye elimu, wanawake warembo, wanaume wenye sura nzuri, watu mashuhuri, wanaojitosheleza kwa yote, na kila kitu kilipoangamia kisichokuwa chini ya hiyo ishara. Amina.

⁹⁰ Ndivyo itakavyokuwa katika Kuja Kwake Mwana wa Mungu, malaika Wake wa kuangamiza atawaangamiza wote wasio na ile Ishara ya ubatizo wa Roho Mtakatifu juu yao, kuonyesha ya kwamba umetambulishwa, na umekufa, wewe mwenyewe, kwa Dhabihu yako, na umezaliwa katika Roho wa Mungu, na umetiwa muhuri pale na Roho Mtakatifu. Mungu mmoja tu, Naye ndiye tu anayesema Neno linalofaa, na Ndilo hili hapa. Hakuna mwingine anayeweza kutoa kitu chochote Kwake. Angalia.

⁹¹ Yeriko ilikuwa imesikia yale Mungu aliyokuwa akifanya. Yeriko ilikuwa imelisikia neno. Unakumbuka vile kahaba huyo alivyosema, “Tulisikia jinsi ambavyo Mungu alifanya mambo makuu. Nahofu. Je! mtaniokoa tu kama nikiwatendea mema?” Yos- . . .

⁹² Na Kalebu na—na—na Yoshua walikuwa wamewaambia la kufanya, jinsi ya kuifunga kamba hii nyekundu, na kukaa chini yake. “Hatuwajibiki kwa mtu mmoja!”

⁹³ Kasema, “Je! naweza kumwingiza baba yangu? Naweza kumleta mama yangu? Naweza kuwaleta ndugu zangu, dada zangu, jirani zangu?”

“Walete wote uwezao chini yake.”

⁹⁴ Ndivyo ilivyo leo, ndugu. Si, “je! tunaweza kuwaleta Wamethodisti? Tunaweza kuwaleta Wabaptisti? Tunaweza kuwaleta Wapentekoste?” Wote walio tayari kuingia chini Yake, Mungu atakukubali wewe. Lakini Hiyo, na Hiyo peke yake, ndiyo itakayokutambulisha tu pamoja na Yeye. Angalia. Naam.

⁹⁵ Nguvu Zake kuu na ishara alizokuwa amefanya kule chini, nao walikuwa wameziona na kuzijua. Kwa nini hatuwezi kuwa na wanawake na wanaume, leo, waaminifu tu kama mwanamke huyo alivyokuwa mwaminifu, tunapooa kile Mungu alichohidi kufanya na kumwona Yeye akikifanya?

Ndipo, jambo linalofuata, ikaja hukumu.

⁹⁶ Hapana budi waliamini walikuwa—walikuwa . . . Waliamini, hapana budi waliamini walikuwa wako salama katika ukuta huo mkubwa walimokuwa, ambamo walikuwa, familia yao kubwa, jumba lao kubwa mno. Watu wengi siku hizi . . .

⁹⁷ Ninasema jambo hili, kwa uchaji na heshima. Watu wengi, leo, wanasema, “Mimi ni mfuasi wa kanisa lililo kubwa sana mjini. Mama yangu alikuwa ni mfuasi wa kanisa hilo. Ni moja ya makanisa yaliyo ya zamani sana kuliko mengine yote.” Hilo halina uhusiano wowote nalo. I—Ishara haina budi kuwekwa!

⁹⁸ Huenda walifikiria, ya kwamba kitu hicho kikubwa walichoishi ndani Yake, mfumo huo mkubwa, ya kwamba ungekwenda kuwaokoa. Bali tunaona ya kwamba, kila kitu ambacho hakikuonyesha ishara hiyo, kiliangamia, katika mji huo. Ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu; Yeye amekwisha kusema hivyo tayari.

⁹⁹ Bila shaka kulikuwa na baadhi ya hao wavulana wa kanda, ama mtu fulani, aliyeingia mahali pale kisiri na kuwachezea baadhi ya kanda, ama kitu kama hicho, na akawapata waliochaguliwa tangu zamani. Alichukua nyumba yake yote, na kuitumia kama kanisa, na kuwapokea hao wajumbe.

¹⁰⁰ Ndipo wakati walipowapata wote, katika mji huo, ambao wangekuja chini yake na kuamini hiyo ishara, wakati alipowaleta wote pale, ndipo maangamizi yakaja. Wakati hasira ya Mungu ilipoangamiza mfumo huo mkubwa waliokuwa nao kule chini, hiyo alama ya ishara iliweka nyumba yake salama. Alama ya ishara, si kitu kingine.

¹⁰¹ Haidhuru ni mashirika mangapi, na ni zana ngapi nzuri za Msalaba Mwekundu walizokuwa nazo, mambo ambayo yote

ni mazuri, ni kiasi gani cha hiki, na ni mashirika mangapi ya msaada, kila kitu kiliangamia kisichokuwa chini ya hiyo ishara. Sasa hebu wazia jambo hilo, kila kitu kiliangamia! Sijali walikuwa na kanisa kubwa jinsi gani, walikuwa wafuasi wa madhehebu makubwa jinsi gani, jinsi gani ikulu ya mfalme ilivyokuwa kubwa; kila kitu kiliangamia.

¹⁰² Na vivyo hivyo ndivyo kila kitu kilivyoangamia Misri, ambacho hakikuwa chini ya ile ishara.

¹⁰³ Sasa, Mungu habadilishi njia Zake. Yeye ana Ishara leo. Ndugu yangu, dada, afadhali uipokee. Afadhali uwe nayo. Kumbuka tu, ni onyo.

¹⁰⁴ Angalia, uhai ule ule ambao ishara hiyo ilifanya, na—na jambo lile lile ambalo i—ishara ilifanya kule Misri, iliokoa kila kitu kilichokuwa chini yake. Kila kitu kisichokuwa nayo kiliangamia.

¹⁰⁵ Yoshua ni mfano wa Yesu. Ambalo, *Yoshua* maana yake ni “Yehova-Mwokozi,” vilevile *Yesu* linamaanisha “Yehova-Mwokozi.” Yoshua alikuwa mwaminifu kwa alama ya ile Ishara ambayo wajumbe wake walikuwa wamehubiri. Vivyo hivyo Yesu atakuwa mwaminifu kwa alama ya ishara ambayo wajumbe Wake walihubiri, wakati Yeye atakapokuja. Wote waliokuwa chini yake waliokolewa, huko Misri. Wote waliokuwa chini yake waliokolewa, huko Yeriko. Na leo je? Tunaona, damu ya mwana-kondoo ilikuwa mfano wa Yesu Kristo. Vema.

¹⁰⁶ Katika Waebrania 13, tunaona jambo hili, linaitwa pale, “Agano la milele.” Mungu alikuwa na agano nao. Lakini ile Damu sasa ni agano la milele, Damu ya Yesu Kristo.

¹⁰⁷ Ahadi za Mungu zilizofungwa kwa Damu zinatuweka huru na dhambi na nafsi zetu, zinatuweka huru na kitu chochote cha ulimwengu. Haidhuru tunajaribu kuutengeneza jinsi gani, ulimwengu, wote umekufa. Kama tuko katika ahadi za Mungu zilizofungwa kwa Damu, hatuoni kitu ila Damu. Wangeweza je kuangalia nje ya mlango huo bila ya kuona ile damu? Unaweza je kuangalia chochote bila ya kwanza kuona Damu ya Yesu Kristo? Kama uko katika Kristo, unaiona Hiyo, kumwabudu Yeye na kuonyesha ahadi zake zenye nguvu. Yeye aliahidi mambo haya kuja. Watu Wake waliofungwa kwa Damu wamo ndani Yake, wametiwa muhuri mle ndani na Roho Mtakatifu, nao wanaangalia tu ile Damu na ile ahadi. Hawawezi kuuangalia ulimwengu. Wamekufa kwa ulimwengu, na ulimwengu umekufa kwao.

¹⁰⁸ Na kuwaona Wakristo, leo, wanaoweza kufanya lolote ambalo walimwengu wengine wanafanya, kutenda kama wao, kuapa kama wao, kunywa kama wao, kuvuta sigara kama wao, na wamezama katika vizimba vya nguruwe vya dhambi, na kumbi za dansi, na vitu kama hivyo, na halafu wangali wanasema ati wao ni Wakristo? Huwezi kufanya hivyo, rafiki.

Hiyo ndiyo sababu watu hawawezi kuamini Nguvu za Mungu, hawawezi kuamini ishara na maajabu, tayari wamekufa kwa mambo Hayo na wa—wamefufukia kule ng'ambo ulimwenguni. Lakini wale waliokufa kwa ulimwengu, wamefufuka katika Kristo na wanatarajia ahadi Yake.

¹⁰⁹ *Agano Jipya* linamaanisha “Mapatano Mapya.” Uhai wa Damu, Uhai wa Damu Yenyewe, ndio ile Ishara. Uhai uliotoka kwenye ile Damu ndiyo ile Ishara. Kumbukeni, katika Agano la Kale, ile damu halisi ya mwana-kondoo ilibidi ipakwe. Hapa, ni Ishara ya ile Damu; ni ule *Uhai uliotoka* kwenye ile Damu, ulio ndani ya huyo mtu, kwa ajili ya ile Ishara. Loo, jamani!

¹¹⁰ Ishara mpya ni ule Uzima mpya unaokuja kwa Yesu Kristo, wakati Damu Yake ilipomwagika, kulitakasa Kanisa na kulijaza na Uwepo Wake, apate kudhihirisha Neno Lake na ahadi Zake kwa watu.

¹¹¹ “Mungu, kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi,” Waebrania 1, ilisema, “alisema zamani na baba zetu katika manabii, lakini katika siku hii ya mwisho katika Mwanawe, Yesu Kristo.” Mwanawe ni nini? Neno. “Neno alifanyika mwili akakaa kwetu.” Na *Huu* ndio Ufunuo, mkamilifu wa Kristo. “Mtu atakayeongeza neno moja Kwake, au kuondoa Moja Kwake, huyo ataondolewa, sehemu yake, kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Huo hapo Ufunuo. Tunahitaji tu Ishara kuwa pamoja nasi kulifanya Neno hilo liishi tena. Hiyo ndiyo sababu ya Yeye kutuma ile Ishara. Inatupa taarifa, inatupa taarifa hiyo, nasi tunajua kwamba ni Kweli.

¹¹² Ile Ishara mpya inaonyesha Yesu ametimiza kila sharti kwa ajili yetu, Naye yupo hapa, Ishara mpya. Ishara ya Roho Mtakatifu inaonyesha ya kwamba tunajua ya kwamba Yesu alikufa apate kutuweka huru na mambo yote ya ulimwengu, na ile Ishara iliyo juu yetu inathibitisha jambo hilo kwa kuthibitisha yale Yeye aliyosema.

¹¹³ Sasa mtu anawezaje kudai kwamba anashikilia hiyo Ishara mbele zake, na kukana kile Neno hili linachosema? Sivyo. Haiwezekani. Mungu hawezi kudanganya kuhusu Neno Lake Mwenyewe.

¹¹⁴ Na kwa sababu Yeye yupo hapa, tuna ha—haki ya vitu vyote alivyotununulia. Angalia, Ishara ilikuwa ifanye nini? Kununua. Ni gharama iliyokwisha kulipwa. Unapokuwa na ile Ishara, una haki basi ya kuonyesha hiyo Ishara, kwa kitu chochote alichokununulia. Wala hakuna mtu anayeweza kununua bila Hiyo. Kinaweza tu kununuliwa na ile Ishara.

¹¹⁵ Kumbuka, kama ulitoka ukaenda hapa nje kwenye shirika la basi, useme, “Njoo, ninawaambia, nina—nina ishara inayosema shirika lingine la basi.” Hilo haliwezekani. “Nina ishara inayosema, inayotoka Maine, kutoka New Hampshire.” Haitafaa huko California. Unapaswa kuwa na ishara ya shirika hilo la

basi, kusudi upate kuinunua. Inaonyesha ya kwamba umelipa nauli hiyo kwenye basi hilo.

116 Na wakati tunapoweza kuonyesha ile Ishara ya Roho Mtakatifu, inaonyesha ya kwamba tumekubalika katika Kristo, na hiyo ndiyo Ishara yetu ya kwamba yote tunayohitaji tayari yamenunuliwa na Yeye. Tumetambulishwa pamoja na Ishara yetu. Ishara haina budi kuwa tayari.

117 Ile Damu, Damu ya Agano, haitambuliwi bila ya ile Ishara. Neno linatuhakikishia ile ahadi. Ile Ishara ni dalili ya kwamba ununuzi umeishafanyika kwa ajili yetu.

118 Utii mkamilifu kwa Neno kamili la Mungu unatupa haki ya kupata ile Ishara. Hakuna njia nyingine iliyopo, ambapo ungeweza kamwe kuwa na haki ya kupata ile Ishara, mpaka utakapotii Neno kikamilifu. Si kile mtu fulani ameweka ndani Yake, na ameongeza Kwake; bali ni yale Mungu aliyosema juu Yake!

119 Wakati Yeye aliposema, “Huna budi kuzaliwa mara ya pili.” Hilo halimaanishi kuruka-ruka madhabahuni; hilo halimaanishi kurudi kule nyuma na kupeana mikono na mchungaji; hilo halimaanishi upuuzi wote huu ambao tumeona ukifanywa; haimaanishi kuandika jina lako kwenye kitabu cha kanisa. Inamaanisha kifo kwa utu wako wa kwanza, na Uzima kwa utu wa pili. Inamaanisha ya kwamba Damu imepakwa, nawe umetambulishwa na Uzima wa Yesu Kristo. Na kama Yeye akiwa ni Mzabibu, nasi tukiwa ni matawi, Uzima ulio kwenye tawi uko pia na unatoka kwenye Mzabibu. Utazaa hilo tunda.

120 Kama tawi hilo la kwanza likichipuka, hilo tawi kutoka kwenye Mzabibu huo, ambao uliandika kitabu cha Matendo nyuma yake; kama tawi hilo likichipuka, Mzabibu ukitoa tawi lingine, wataandika kitabu kingine cha Matendo nyuma yao, maana ni Uhai ule ule. Kama mmoja wa mizabibu yenu nje huku ikizaa zabibu za bluu, kama ukizaa tawi lingine, litazaa zabibu za bluu.

121 Nami nawaambia, leo, tuna mizabibu mingi sana iliyopandikizwa ndani Yake, pamoja na madhehebu na kanuni za imani na kadhalika, na hata hivyo tunda lolote la matunda chungwa lililopandikizwa linaweza kuishi, kuishi katika Mzabibu huo. Bali linazaa tunda lingine.

122 Tunachohitaji, leo, ni ubatizo mwingine wa Roho Mtakatifu, na kuwa na Nguvu halisi za Mungu zinazotambulisha kazi ambazo Yesu Kristo aliahidi kwa siku hii, si sana sana kama siku ile. Siku hii, ile ahadi aliyoitoa hapa. Hiyo ndiyo aliyoahidi kule, Yeye angemmwaga Roho Wake. Sasa Yeye ameahidi jambo hilo tena katika siku za mwisho, na yale ambayo Yeye angefanya.

123 Ni ajabu, ya kwamba daima tunaweza kuangalia nyuma, bali kamwe hamwangelii mbele. Hivyo ndivyo ilivyo na mwanadamu. Daima yeye anasema, anamtukuza Mungu kwa ajili ya yale

aliyofanya, anamsifu kwa yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya. Hivyo daima ndivyo ilivyo kwa mwanadamu. Lingali ni jambo lile lile.

¹²⁴ Utiifu mkamilifu kwa Neno unamleta Mungu, Neno la Milele, ndani yako, na hiyo ndiyo Ishara. Wakati Neno linapokuwa ndani yako, ni Kristo ndani Yako.

¹²⁵ Sasa angalia wakati, basi, wakati tunapoomba, kama tuna ile Ishara. Na wakati tunapoomba, tukiwa na ile Ishara, tu... ama tunaonyesha Ishara yetu pamoja na maombi yetu. Sasa, kama wewe ni mgonjwa, kama wewe ni mwenye dhambi, kama una haja, unapokuwa na ile Ishara, una haki. Kama nilikuwa na Ishara ya shirika la basi, mkononi mwangu, hawawezi kunitoa kwenye basi hilo, wamekubali pesa zangu, nami nina ishara. Katika suala hili, nisingeweza kulipia gharama yangu, wewe usingeweza kuilipia, bali Yeye alitulipia na akatupa hiyo Ishara. Amina. Nina haki ya uponyaji wa Kiungu; Yesu Kristo alikufa ili niweze kuwa na uponyaji wa Kiungu. Nina haki ya kudai kila ahadi kwenye Kitabu hicho. Wakati, unaipata wakati gani? Unapokuwa na ile Ishara na unaweza kuionyesha hiyo Ishara pamoja na maombi yako. Kama hunayo... Ishara ya utiifu mkamilifu; nauli imelipwa.

Paulo anatwambia, “Damu inanena.”

¹²⁶ “‘Damu hunena,’ ati tulisema? Je! Damu hunena? Je! inaweza kunena? Ile Ishara inene?” Naam, bwana.

¹²⁷ Kama tungeninii—tungeangalia katika Mwanzo 4:10, “sauti ya damu ya Habili ililia dhidi ya Kaini.” Tunaona, katika Waebrania 12:24, ya kwamba “Damu ya Yesu Kristo inanena mambo mema zaidi.” Damu hunena! Damu yenyewe inawezaje kunena? Ni ule Uhai, ambao uko katika ile Damu, ndio unaonena. Nafsi iliyokuwa ndani ya Kaini iliyolia, hiyo... ama katika Habili. ilikuwa ni ule Uhai uliokuwa ndani ya Kristo ambao hunguruma mambo mema zaidi kuliko wowote ule! Inanena, na inanena kwa sauti kuu. Ni Roho Mtakatifu. Hunena dhahiri, Yeye anatwambia ya kwamba wakati umewadia. Tunapona jambo hilo mahali Yeye aliposema lingesemwa, halafu tuone akirudi na kudhihirisha yale Yeye aliyosema, ni kwamba, hakuna kitu kingine kilichosalia ila kumwamini, hiyo ni kweli, kuipokea.

¹²⁸ Amini kwa ajili yako mwenyewe, na upake Ishara pia kwa ajili ya familia, kama walivyofanya kule Misri, na kama walivyofanya kule Yeriko. Matendo 16:31, tunaona, Paulo alimwaambia yule—yule Mrumi kuninii, “Ukabatizwe, ukiliitia Jina la Bwana,” yeye na nyumba yake wangeweza kuokoka kwa kufanya jambo lile lile.

¹²⁹ Toka nje! Watu wengine wanataka kupaka ile Damu na wakae ndani. Unapaka Damu na kutoa takataka zote nyumbani, na uwe na wakati wa kuisafisha nyumba. Ninyi wanawake

vueni hizo kaptura. Ninyi wanaume tupilieni mbali hizo sigara; na ninyi wanawake, pia. Ondeleeni mbali upuuzi huu wote wa kale kutoka kwenye mfumo huu hapa, unaoitwa dunia. “Ukiipenda dunia, mambo yaliyo katika dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako.” Unapokuwa uko tayari kupaka hiyo Ishara, toa yote yaliyo ndani yako na uwe tayari kwa ajili ya Hilo. “Huwezi kumtumikia Mungu na mali wakati huohuo.” Wanawake wanakuja . . .

¹³⁰ Nimepitia humu nchini. Nimetoa matamshi kuhusu Bibi Kennedy, akiwa na mtindo wake wa kukata nywele wa Yezebeli, na yote namna hiyo, na afro zake kubwa, na wanawake hawa. Sijui, kama Bibi Kennedy angalikuwa amesikia Jumbe ambazo nimehubiri, huenda angaliachilia nywele zake zikue, wakati mrefu uliopita. Lakini nimepita nchini humu, huku na huko, nikionyesha kwa Neno, ya kwamba ni makosa, na ni hukumu kwa wanawake kukata nywele zao, na wanawake wa Wapentekoste wanaendelea, wanaendelea vivyo hivyo. Huenda yeye akasimama katika siku ya Hukumu, bila kujua jambo hilo, bali ninyi mnajua vyema. Inaonyesha ya kwamba ile Damu haijapakwa. Ile Ishara haipo.

¹³¹ Nywele ndefu ni nadhiri ya M—Mnazarayo. Lilionyesha ya kwamba umejiondoa ulimwenguni, upate kutii Neno. Amina. Samsoni aliachilia nywele zake zikue, kama nadhiri ya Mnazarayo. Sasa sisi tunayatambua mambo haya.

¹³² Na wanawake wakivaa na kutenda na kufanya, na waume wakiwaruhusu kufanya jambo hilo, kundi kubwa la madondoadume! Inaonekana kana kwamba hakuna mwanamume tena. Unawaona wanaume wakivaa viatu vya waridi, na—na ni wahubiri mimbarani, kitu kama hicho. Hiyo ni fedheha. Ninapenda kumwona mwanamume tena ambaye ni mwanamume kabisa. Inaonekana kana kwamba kuna nguvu fulani zinazowasukuma kufanya jambo hilo, ni ibilisi na ushawishi wa siku hii. Hiyo ni kweli. Mara nyingine mwanamume mwenye uzito wa ratili mia mbili, na misuli namna *hiyo*, wala hakuna hata wakia moja ya mwanamume ndani yake; anatenda mambo kama dondoadume fulani kubwa nje huku. Ninapenda, acha mwanamume awe mwanamume. Acha wanawake wafanye kama wanawake, acha wawe mabibi. Wakati ile ishara inapopakwa, wanaarudi kuwa hivyo. Mungu aliwaumba tofauti, nao ni tofauti. Wanaume wanataka kuonekana kama wanawake; wanawake wanataka kuonekana kama wanaume.

¹³³ Inaonyesha kuna upotovu, roho nyeusi inayoning’inia kule, giza nene juu ya watu. Ni wakati wa kuitwa kutoka. Kulikuwa na giza juu ya Misri, kabla ya kule kuitwa kutoka, ndipo ile ishara ikapakwa. Wakati wa kanisa kupata ile Ishara umewadia, la sivyo giza nene liko juu ya watu. Giza nene!

¹³⁴ Naam, isafisheni kabati, isafisheni nyumba hii, loo, tuna kusafisha nyumba kwa mtindo wa kale! Damu na ipakwe, na ndipo Ishara itaingia. Isafisheni kabisa! Itakaseni!

¹³⁵ Ndipo pakeni ile Ishara katika Maombi, kwa ujasiri, utakapokuwa umejisafisha kabisa. Umeachana na jambo la ulimwengu. Umetupilia mbali kutokuamini kote. “Sijali watu wanasema nini. Kama Neno la Mungu linasema jambo hilo, na liliahidi, ninaliamini. Kama Neno linasema jambo, hilo latosha. Sijali yale mtu mwingine yeyote anayosema.” Unaona? Ndipo wakati umekwisha kufanya mambo hayo yote, umepaka Damu na unaamini kila Neno, ndipo uchukue Ishara yako katika maombi, ushawishike kabisa.

¹³⁶ Tunasoma katika—katika Waefeso, mlango wa 2 na kifungu cha 12, juu ya yale Mungu aliyosema kuhusu jambo hilo, tulipopaka Ishara hii. Angalia, “kumtumikia Mungu aliye hai,” kwa matendo yaliyo hai, na kwa ishara zilizo hai, kwa Ishara hai. Si matendo mafu, na ya kimwili, si matendo mafu. Waebrania 9:11-14, inatwambia tena, jambo lile lile. Si kanuni za imani zilizokufa; bali ni Ishara iliyo hai! Hizo, kanuni hizi za imani, zinakana ya kwamba kuna kitu kama Ishara. Hata haziamini kuna kitu kama Ishara, ubatizo wa Roho Mtakatifu.

¹³⁷ Lakini sisi tunaamini Neno, tunapambanua, tunajua, na ni Uwepo Wake ulio hai kwa ajili yetu siku hii. Tumejitenga na matendo mafu, ndipo Roho Mtakatifu anaingia kuthibitisha Neno na kulifanya dhahiri. Waebrania 13:8 inathibitisha jambo hilo kwetu, inathibitisha ya kwamba Mungu amemfufua kwa ajili yetu, kulingana na Neno Lake lililoahidiwa. Maelfu ya miaka imepita, miaka elfu mbili, karibu hiyo, imepita, bali (ni kitu gani?) ile Ishara ingali inashikilia, ya kwamba Mungu alimfufua katika siku ya tatu. Kama una Neno tu, hilo tu ndilo ulilo nalo. Lakini ile Ishara inapopakwa, ndipo Kristo anakuwa ni halisi kwako, Naye anafanya leo kama alivyofanya wakati huo. Na kwa hiyo linalitupa moja kwa moja pajani mwao tena; hawawezi kuliepa. Mungu aliliahidi, Nalo ndilo hili hapa. Lakini, ile Ishara haina budi kupakwa, wewe chukua ile Ishara.

¹³⁸ Na wakati—na wakati unapokubali Damu Yake ya sadaka, ndipo Yeye hutupa sisi Uhai, Uhai wa ile Ishara, na huo ni Muhuri ulioahidiwa. Waefeso 4:30, “Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mliwiwa muhuri mpaka siku ya ukombozi wenu.” Basi, mkiisha kubatwiza ndani Yake, Wakorintho wa Kwanza 12, tumekuwa sehemu ya Mwili Wake.

¹³⁹ Na ndani Yake ndio kuwa na utimilifu. Ndani Yake ni utoshelevu wote tunaohitaji. Yeye ni raha yangu. Yeye ni Uzima wangu. Yeye ni furaha yangu. Yeye ni ninii yangu. . . Yeye ni zaidi. . . Si, sina haja ya kuvuta sigara nipate namna fulani ya faraja. Ninachukua Ninyoro ya Bondeni. Yeye ndiye bangi. Yeye ndiye kitu ambacho—ambacho kinanifanya nibubujike

kwa furaha. Yeye ndiye anayenitosheleza kwa yote. Yeye ni matumaini yangu. Yeye ni raha yangu. Yeye ni Mungu wangu. Yeye ni Mwokozi wangu. Yeye ni mponya wangu. Yeye ni mambo yote ninayohitaji. Kwa sababu, ninakufa, tunakufa ndani Yake, na tunabatizwa ndani Yake, na ndani Yake kuna utoshelevu wote.

¹⁴⁰ Sikilizeni kwa makini wakati nikitoa matamshi haya ya kufunga. Kama Shetani akijaribu kukupa takataka hizi, kama vile magonjwa, unajua la kufanya? Mwonyeshe tu ile Ishara. “Mimi ni bidhaa iliyonunuliwa. Uponyaji wangu umelipiwa. Mimi ni tunda la Mungu, kwa kuwa nina Ishara ya Roho Mtakatifu. Huwezi kuniondoa kwenye Barabara hii kuu. Huwezi kunizuia nisipate afya yangu. Ninakuonyesha ile Ishara na kukuonyesha ya kwamba ninii yangu... ‘Kwa mapigo Yake mimi niliponywa.’ Huu hapa ufufuo wa Yesu Kristo, papa hapa ndani yangu sasa, kukuthibitishia huo.” Loo, hicho hapo kitu halisi! Hiyo hapo ile Ishara.

¹⁴¹ Hiyo ndiyo sababu watu hawaiamini. Hiyo ndiyo sababu ni vigumu kwao kuona ndani. Ile Ishara haijawahi kamwe kupakwa. Unaona, hiyo ndiyo sababu, wanasema, “Loo, siku za miujiza zimepita.” Unafanya hivyo kwa upofu.

¹⁴² Yesu alisema, “Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa; asieyeamini atahukumiwa. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Umbali gani? “Ulimwenguni kote, kwa kila kiumbe.” “Kwa Jina Langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Weka hiyo Ishara, ndipo udai haki zako. Itikise mbele za Shetani!

¹⁴³ Dereva wa basi anasema, “Aisee!” Mtu wa ndege anasema, “Aisee! Huwezi kuingia kwenye ndege hii.”

“Hiyo hapo ile ishara.” Amina!

¹⁴⁴ “Wewe ni fukara sana. Wewe si ninii... Wewe ni matambara. Wewe ni maskini sana. Sisi hatuchukui watu duni, tunachukua watu maarufu.”

¹⁴⁵ “Lakini mimi nina tiketi.” Amina! “Huwezi kunikataza kuingia.” Haleluya! “Wanaponipa hiyo tiketi, hiyo inatosha.”

¹⁴⁶ Nina haki, kama waliyo nayo wengine. Nina haki, kama tu vile Paulo alivyokuwa nayo. Nina haki, kama ile ya mtu yeyote aliyepata kubatizwa kwa Roho Mtakatifu aliyo nayo. Nina haki ile ile, kwa maana nina Ishara ile ile, kumwonyesha Mungu yeye yule alichonunua kwa Kitu kile kile, siku ile ile, kwenye kitu kile kile.

¹⁴⁷ Haya basi, ile Damu, ile Damu! Ile Ishara, si Damu yenyewe, bali ni ile Ishara, Roho Mtakatifu, Uhai uliotoka kwenye ile Damu, ambao huja. Huo Uhai hufanya nini? Unakuja na

kuthibitisha kile ile Ishara ilichonunuliwa kwa sababu hiyo. Ile Ishara inathibitisha kile ile—ile Damu ilichokununulia. Damu ilinunua ukombozi Wako. Ile Ishara ni thibitisho Lake. Ile Damu, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, alichubuliwa kwa uovu wetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Unaona, yote ni Damu, Damu, Damu! Ndipo wakati ile Ishara inapokuja, inaonyesha ya kwamba umetambulishwa pamoja na Sadaka yako. Amina! Ibilisi hawezi kukuzuia hilo.

¹⁴⁸ Hapo ndipo ninaposimama mimbarani hapa, kukabiliana na kila kitu kilichopo, na kote ulimwenguni, na pepo. Neno la Mungu liliahidi jambo hilo. Mradi tu ninaweza kujua ya kwamba Damu imepakwa, na nikimshikilia huyo Roho Mtakatifu hapa moyoni mwangu, ibilisi hana hata neno moja la kusema dhidi yake. Naam, bwana.

¹⁴⁹ “Tutatembea ambapo mitume wamekanyaga,” naam, bwana, kwa sababu ile Ishara imelipia hiyo njia. Ishara hiyo ndiyo thibitisho ya kwamba safari imelipiwa, na tumeikubali. Na, ili kuthibitisha jambo hilo, Mungu alitupa ile Ishara, ishara ya kwamba tulipokelewa.

¹⁵⁰ Mhudumu mmoja aliniambia wakati mmoja, alisema, “Ndugu Branham, Ibrahimu alimwamni Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Kasema, “Mtu anaweza kufanya nini cha zaidi ila kuamini?”

Nikasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

¹⁵¹ “Basi unampata wapi huyu Roho Mtakatifu, nje ya kuamini?”

¹⁵² Nikasema, “Lakini Yeye alimpa muhuri wa tohara, kama thibitisho la imani yake.” Amina.

¹⁵³ Na kama Yeye kamwe hajakupa ubatizo wa Roho Mtakatifu, bado, basi Yeye hajathibitisha imani yako unayosema kwamba unayo. Lakini ile Ishara ndiyo thibitisho.

¹⁵⁴ Ninasema, “Nina pesa, nilizilipia ofisini pale chini!” Lakini inakupasa kuonyesha ile ishara. Hiyo ni kweli. Ninapoonyesha ishara, nina haki.

¹⁵⁵ Na wakati ninapoweza kuonyesha ile Ishara, ya Roho Mtakatifu, una haki ya kupata kitu chochote kilichonunuliwa ambacho Yesu alikifia. Ni Ishara. Hebu angalia kwa muda mfupi tu, tunapofunga. Shikilia Ishara hiyo juu ya imani yako isiyo na mashaka katika Neno lililoahidiwa. “Ninaamini ya kwamba Yesu alisema, ‘Mkimwomba Baba neno lolote katika Jina Langu, nitalifanya.’” Shikilia Ishara yako juu ya Neno hilo lililoahidiwa, na utembe moja kwa moja kwenda kwake. “‘Mimi ni Bwana nikuponyaye magonjwa yako yote.’ ‘Alijeruhiwa kwa makosa yangu, kwa mapigo Yake niliponywa.’ Ninachukua Ishara yangu,

ya Roho Mtakatifu aliye ndani yangu, na naishikilia juu ya maombi yangu, na kusema, 'Bwana Mungu, Wewe uliahidi jambo hilo, "Nitakapoiona ile Ishara, nitakujazi. Niliahidi kufanya jambo hilo."'" Hawezi kufanya jambo lingine lolote. Yeye anaangalia moja kwa moja kupitia kwenye Damu ya Mwanawe. Hiyo hapo Ishara imepakwa. Hana budi kufanya hivyo kwa sababu aliahidi.

¹⁵⁶ Asingeweza kuingia ndani ya nyumba, yule malaika wa mauti, mwangamizi, na kumchukua mtu mmoja. Asingeweza kufanya hivyo, kwa maana kulikuwa na damu ya mwana-kondoo, masharti ya Yehova.

¹⁵⁷ Na masharti Yake, leo, ni Damu ya Mwanawe Mwenyewe, Yesu Kristo, na ile Ishara ya Roho Mtakatifu.

¹⁵⁸ Hatuna Hiyo; huenda tukawa sisi ni Baptisti, Presbiteri, Lutheri, Wapentekoste, chochote kile tungekuwa; huenda tukapaza sauti, tukapiga makele; huenda tukawa, loo, na elimu sana. Hilo halina uhusiano wowote na jambo hilo. Inakupasa kuonyesha ile Ishara.

¹⁵⁹ Ndipo, wewe uko kwenye ufufuo, kwa maana Nguvu za ufufuo zimo ndani yako tayari. Ile Ishara ndiyo Nguvu za kufufuka, ikionyesha ya kwamba Yesu alifufuka katika wafu. Na wewe umefufuka katika wafu, mambo yaliyokufa ya kutokuamini, na umefanywa hai katika Neno la Yesu Kristo. Unaamini jambo hilo na hilo Neno linaishi kupitia kwako.

¹⁶⁰ "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu likae ndani yenu, ombeni mtakalo." Yohana 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya; kubwa kuliko hizi atazifanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba." "Bado kitambo kidogo, na ulimwengu haunioni tena; hata hivyo mtaniona, kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu." Alifanyaje hivyo? Si ule mwili; unaketi kwenye mkono wa kuume wa Ukuu. Bali ni ile Ishara, ya kwamba wewe umempokea, Naye amekurudishia Hiyo, chukua Ishara hiyo na udai kitu chochote unachotaka. Mungu aliahidi hilo.

¹⁶¹ Daima nimesema, nilikutana na tabaka mbili za watu: wa kimsingi, na Wapentekoste. Wa kimsingi, mahali pao, husoma Maandiko na kuyawazia. Wanasema, "Vema, sisi ni wana wa Mungu." Wanaamini jambo hilo, naam, bwana, lakini hawana imani yoyote kuendana na jambo hilo. Lakini Wapentekoste wana imani nyingi sana, nao hawajui wao ni wana wa Mungu. Ni kama vile mtu aliye na pesa kwenye benki, hawezi kuandika cheki; na huyo mwingine anaweza kuandika cheki, ila hana pesa kwenye benki.

¹⁶² Kama ukiwahi kuweka kitu hicho pamoja, mpaka wanaume na wanawake wangeweza kutambua! Ninyi ambao kweli mmebatizwa katika Roho Mtakatifu, nanyi mna ile Ishara mnayoweza kuonyesha, mna haki kwa kila baraka za ukombozi

ambazo Mungu aliahidi. Kila kitu alichohidi, ni chako. Shikilia Ishara yako juu ya imani yako isiyo na mashaka, unapoomba, na juu ya Neno Lake. Imani katika Neno Lake!

¹⁶³ Mungu wakati mmoja aliwapa watu Ishara, na hiyo ilikuwa ni upinde wa mvua. Angalieni, sikilizeni kwa makini; tunafunga. Mungu daima alidumu mwaminifu kwa ishara hiyo. Huko nyuma kabisa katika siku za Nuhu, kwenye yale maangamizi ya ulimwengu uliokuwapo kabla ya ile gharika, Mungu alilipa taifa hili, ama aliupa ulimwengu, ishara ya upinde wa mvua, kama ishara. Na Mungu daima anaionyesha ishara Yake, huku maelfu ya miaka ikipita. Yeye kamwe hashindwi, kwa maana Yeye huziangalia ishara Zake. Maelfu yote haya ya miaka, Yeye ametuonyesha hiyo, akituonyesha ya kwamba Yeye hashindwi kamwe kuheshimu ishara. Yeye kamwe hashindwi kuihashimu.

¹⁶⁴ Yeye anatatara jia sasa kuonyesha Ishara juu ya imani yetu, kwa kundi la Shetani, na wasioamini, na madhehebu, na kadhalika, wasioamini Hiyo; ya kwamba sisi tunaoamini yale Yeye amesema kuhusu ahadi Zake, na ya kwamba Yesu Kristo amefufuka kutoka kwa wafu, akijionyesha Mwenyewe kwamba yu hai. Na hiyo ndiyo beji, ile Ishara ya utambulisho, kwa maana ni Maisha ya Kristo Mwenyewe ndani yako, akitambulisha Neno. Halihitaji kitu kingine chochote.

¹⁶⁵ Hiyo ndiyo Ishara. Bila Ishara...Inaonyesha nauli imelipwa! Inaonyesha ya kwamba wewe uko kwenye ufufuo! Ya kwamba Mungu, Nguvu zile zile zilizomfufua Yesu toka kaburini, wewe unazishikilia ndani yako, kama ile Ishara. Roho Mtakatifu, ndani yako, ni Ishara inayokuleta kutoka kaburini. Kwa sababu, hiyo Ishara ni Mungu, Roho Mtakatifu, ambaye ni Uzima wa Milele. Linatoka katika neno la Kiyunani, *Zoe*, ambalo maana yake ni “Uhai wa Mungu Mwenyewe” ndani yako. Na hicho ndicho kitu pekee kinacholipia hiyo gharama. Kama Ishara hiyo haipo, utafufukaje?

¹⁶⁶ Ndugu, dada, usiku wa leo, kwa kumpa Mungu haki yote pamoja na kwa Neno Lake, na sisi kwa sisi, na kwa wakati tunaoishi sasa! Kama wewe huna hiyo Ishara, endapo huna ile Ishara, huenda baadhi yenu hata msiiamini, bali ipo hapa. Ishara imekuwapo hapa tangu Kristo alipokufa. Mbona usijitambulishe, katika mauti kwa mawazo yako, usiku wa leo, na uruhusu mawazo yaliyo ndani Yake yawe ndani yako? “Mawazo ya moyo wangu na yapate kibali Kwako, Ee Bwana. Neno Lako na linini...” “Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu,” hiyo ni Yeye, “basi ombeni mtakalo nanyi mtapewa.” Hivi hamwamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶⁷ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

168 Ni watu wangapi humu ndani wanaojua, ya kwamba jinsi unavyoishi, ya kwamba kweli hujaipaka hiyo Ishara, unajua haiko? Unaiamini, unaiamini kabisa; bali huna, unajua huna? Waweza tu kuinua mkono wako, useme, “Niombee, Ndugu Branham”? Hebu vichwa vyote viinamishwe. Mungu awabariki.

169 “Sinayo. Sina, Ndugu Branham. Nilijaribu kuikubali. Ninaiamini, bali kweli haijapakwa kwangu bado. Ninaangalia katika kioo, ninaona ya kwamba mimi siko. Ninaangalia jinsi ninavyo—ninavyojisikia, kile kilicho nafsini mwangu, nimejaa hamaki, hasira, nina wivu. Nina ninii yote...” Loo, jamani! Hayo yangemhuzunisha Roho Mtakatifu akuache, sasa hivi. Unaona? Unaona?

170 “Nami nawaambia, ni—ni—ninafanya, ninaliona Neno na kuliona linathibitishwa; bali hata hivyo ni—nina kundi tu la watu ninaoambatana nao, kwenda kanisani mwangu, ama shirika langu, karamu yangu ya kadi, ama chochote kile. Siwezi kuacha hayo kamwe.”

171 Hiyo inaonyesha ya kwamba huna ile Ishara. “Ukiipenda dunia, au mambo yaliyomo duniani, kumpenda Mungu hakumo...” “Tokeni kati yao,” Biblia ilisema, “msiguse vitu vyao vilivyo vichafu.”

172 Enyi marafiki, haliwezi kufanywa halisi zaidi kuliko lilivyo sasa. Haliwezi. Ishara iko hapa, kama tutaiamini. Je! mnaiamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Tafadhalini ikubalini. Sawa.

173 Bwana Yesu, wako mikononi Mwako sasa. Jalia ile Ishara, ile Ishara, ya kwamba Yesu si mfu; ile Ishara, ya kwamba Yesu alifufuka kutoka katika wafu na yupo hapa usiku wa leo. Yeye ni Ishara ya kufufuka Kwake. Yeye Mwenyewe ni Neno. Yeye yupo hapa kuthibitisha kila kitu alichosema. Yuko hapa kuthibitisha kila ahadi aliyotoa. Laiti watu wangaliweza kuiona tu mara moja, Bwana, ya kwamba si kitu ambacho tungekisia juu yake. Ni kitu ambacho hatuna budi kujua, Bwana. Hakuna “kujaribisha tena,” huwezi kurudi na kujaribu tena. Linapaswa kufanywa sasa. Ninaomba, Mungu, ya kwamba kila mtu atampokea, usiku wa leo, na jalia ile Ishara ya Damu ipakwe kwenye kila moyo. Na kisha jalia kuwe na ufufuo utakaokuja kupitia katika nchi hii hapa, utakaokuwa mkuu. Baba, tunalikabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

174 Sasa wakati tukiwa katika maombi, kila mtu sasa anyamaze kimya, mtu yeyote asisogee sasa, hebu kidogo.

175 Je! Mnaamini hii ni Kweli, ya kwamba ishara haina budi kuonyeshwa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ililazimu, katika kila wakati, kila kipindi, ilibidi ionyeshwe.

176 Sasa, kwamba Ishara ni nini, ni thibitisho la Neno Lake. Ambayo, ambayo inaonyesha Yeye ni Neno. Sasa, Neno lilisema

ya kwamba Yeye alifufuka toka kwa wafu, Naye yu hai milele na milele. Yeye anaishi ndani ya watu Wake, yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama unaamini jambo hilo, basi una haki; kama una hiyo Ishara, Roho Mtakatifu, ndani yako, una haki ya kila kitu ambacho mauti Yake ilinunua kwa ajili yako. Hivi huwezi kuamini jambo hilo? Sasa, angalia, kwa hiyo. . .

¹⁷⁷ Sasa, usiku wa leo, hatukuwa twende tukawaombee wagonjwa, usiku wa leo. Tutafanya hivyo kesho alasiri. Lakini tuna—tunaninii, usiku wa leo, tulikuwa twende kufanya wito huu wa madhabahuni.

¹⁷⁸ Hapa, wapendwa. Kama ulipata kuponywa, kama ukiishi muda mrefu vya kutosha utakuwa mgonjwa tena. Lakini kama wakati mmoja utachukua hiyo Ishara, umekuwa nayo milele. “Msimhuzunishe yule Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa Yeye mmetiwa muhuri hadi siku ya Ukombozi wenu.” Si hadi ufufuo ufuatao; hukutiwa muhuri; ulipata mchocheo wa mhemuko. “Bali mmekufa, na uhai wenu umefichwa katika Mungu, kwa njia ya Kristo, nanyi mmetiwa muhuri na Roho Mtakatifu.” Kama umewahi kubatizwa na Roho Mtakatifu! Sasa, unaweza kurudi nyuma, hiyo ni kweli. Bali huwezi kuondoka kwenye muhuri huo. Umetiwa muhuri ndani Yake.

¹⁷⁹ Sasa kama huna muhuri huo, hebu na tuwe waaminifu kabisa. Tuna mahali palipoandaliwa hapa, na, kwa kila mtu, tunaweza kumpokea Roho Mtakatifu. Na kama Yeye huwaponya wagonjwa. . . Kwa nini basi akaweka jambo hilo moyoni mwangu kufanya jambo hili?

¹⁸⁰ Sasa, Yesu yeye huyo, aliyefufuka toka kwa wafu, yupo papa hapa sasa. Sasa sikilizeni. Neno haliwezi kusema jambo moja na kumaanisha lingine. Yeye alisema, “Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, Mimi nipo hapo katikati yao.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁸¹ Sasa angalieni upande huu, mnapofanya hivyo. Ni wangapi waliopo hapa ndani ambao ni wagonjwa, inueni mikono yenu. Sema tu, “Mimi ni mgonjwa, mimi ni mhitaji, ama mimi. . .” Haikubidi kuwa mgonjwa. Sema tu, “Nina haja ya Mungu. Ndugu Branham, nina haja ya Mungu, kwa ajili ya jambo fulani. Ni—ni—ninaamini Yesu yupo hapa.”

¹⁸² Sasa shikilia Ishara yako papo hapo juu ya shauku hiyo. Sasa hebu niwaambie, kwa Neno Lake, Yeye—Yeye hawezi kwenda kinyume na Neno hilo. Yeye tayari amekwisha kununua shauku yako, kama ni kulingana na mapenzi Yake. Na mapenzi Yake ni kuponya. Mapenzi Yake ni kukupa shauku yako. “Hatawanyima mema wale wanaoenda sawasawa mbele Zake,” wakionyesha hiyo Ishara.

¹⁸³ Sasa, hatufahamiani na ninyi. Lakini, hebu kidogo, mpate kuona. Sasa hawa hapa wahudumu wameketi nyuma yangu,

watu kila mahali. Kuna kuamini na kutokuamini hapa, daima hivyo ndivyo ilivyo. Unaweza kukusikia kukiingia. Lakini ni upako wa Roho Mtakatifu, na huyo Roho Mtakatifu ndiye ile Ishara. Yeye ndiye hiyo Ishara.

¹⁸⁴ Sasa, haikubidi kufanya jambo hilo. Kila mtu hakuwa Musa, kulikuwa na Musa mmoja, bali watu waliifuata. Sasa hebu amini tu jambo hili, ya kwamba Yeye yu hai leo. Yeye yupo hapa kama shahidi. Sasa kila mmoja wenu una kitu fulani moyoni mwako. Omba.

¹⁸⁵ Sasa, kama Yeye angekuwa yupo hapa, ungesema, “Bwana Yesu, je! utakuwa radhi kuniponya?” Angesema, “Tayari nimelifanya jambo hilo.” Unaona, asingeweza kufanya hivyo tena. Amekuponya tayari, bali anataka tu wewe uamini.

¹⁸⁶ Sasa, Yeye aliahidi, katika siku za mwisho, ya kwamba yale Mungu aliyofanya katika mwili wa kibinadamu, kabla tu ya Sodom, mwishoni mwa siku za Umataifa, lingejirudia tena. Yeye aliahidi hilo. Je! sasa ataitimiza ahadi hiyo?

¹⁸⁷ Yeye aliahidi, Malaki 4, ya kwamba angefanya jambo hili, na kulidhihirisha Neno Lake, “kuigeuza mioyo ya watoto iwarudie baba zao tena,” kurudi kwenye Neno asili la pentekoste, Neno halisi la Biblia. Si ninii . . .

¹⁸⁸ Ya Kipentekoste, wao wanadai, madhehebu ya Kipentekoste, “Hakuna kitu kama hicho.”

¹⁸⁹ Pentekoste ni tukio, si madhehebu. Walijaribu kuiundia madhehebu, bali huwezi, unaona. Haiundiwi madhehebu. Pentekoste ni tukio, ni Muhuri wa Mungu, Roho Mtakatifu aliyeshuka kwenye Siku ile ya Pentekoste.

¹⁹⁰ Sasa ninyi aminini. Angalieni huku na mwamini ya kwamba nimewaambia Kweli. Na kama Yeye atajidhihirisha Mwenyewe; sijui kama atajidhihirisha ama la. Lakini, kama atajidhihirisha, hiyo itaonyesha ya kwamba, ile Ishara ninayonena habari zake, ya kwamba Damu imekwisha kupakwa, na ile Ishara iko hapa kuthibitisha ya kwamba hiyo Damu ni jambo la kweli, ya kwamba Yesu Kristo amefufuka toka kwa wafu. Je! mnaamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema, hilo, vipi, je! inaweza kuwa dhahiri zaidi ya hapo? Unaona? Amini tu Hilo.

¹⁹¹ Ndugu, dada, na marafiki, katika Jina la Yesu Kristo, aminini Hilo, kwa ajili ya nafsi yenu na kwa ajili ya wengine. Kamwe hamtakuwa na nafasi nyingine.

¹⁹² Kama Mungu angalisema nami huko nyuma kabla ya kuwekwa misingi ya dunia, wakati nilipokuwa wazo niani Mwake, na ndivyo ulivyokuwa na wewe pia, kama angalisema, “Je! ungetaka kuishi katika wakati gani?” Ningalisema sasa hivi. Huu ndio wenyewe kabisa, wakati mzuri zaidi uliopo.

¹⁹³ Amini, sivyo? Sasa, ili mpate kujua ya kwamba Yesu Kristo yu hai. Sasa ninii tu, moyoni mwako, omba, na useme, “Bwana, Wewe ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana na hali yetu ya udhaifu, nami ninaamini ya kwamba Wewe ndiwe ile Ishara. Sasa sema na mimi, nipate kuponywa.”

¹⁹⁴ Mtu fulani, na mwende kwa sehemu-sehemu, namna hiyo, unaweza kuona ni wapi, ili kwamba isinilazimu kuwa nikigeuka huku na huko, upande *huu*. Unaona nyakati . . .

¹⁹⁵ Unaona, ono, unapoona ono, halina budi kufasiriwa, pia. Limegeuka. Kwa hiyo, kwa hiyo wakati mwingine wakati una mamia ya wanaovuta, unaweza tu . . . na haina budi kuchukua mmoja tu.

Sasa, kila mtu awe na kicho sana kwa dakika chache tu.

¹⁹⁶ Halafu, hiyo itathibitisha. Kama mtu akisema jambo lolote, na—na—na Mungu haliungi mkono, vema, basi isingeweza kuwa ni Mungu. Lakini kama Mungu akiliunga mkono, basi ndiye utakayesema naye, juu ya jambo hilo. Na litukie kwa utukufu wa Mungu, ninaposimama hapa kuwakilisha kwamba Neno hili ni Kweli.

Yupo mtu anayeketi moja kwa moja pale. Kama ukininii . . .

¹⁹⁷ La—laiti mngeweza kuona katika kiwango hiki, Nuru hii. Sasa, sasa hivi . . . Unaona, jambo fulani lilitukia; Yeye aliivuta akaitoa, kama inavyokuwa sehemu ya mwanadamu ikikaa kando. Hicho ni kipawa. Na wakati kinapofanya hivyo, basi ni—ni ulimwengu mwingine.

¹⁹⁸ Yupo mtu anayeketi pale, naye anaomba. Na, ana shida gani, ameshafanyiwa upasuaji ama kitu fulani, kwenye utumbo. Na imekuwa ni muda mrefu uliopita, bali hauendelei vizuri. Natumaini hatalikosa. Lakini Mungu atanisaidia, nitaita jina lake. Bw. Price, naamini sikujui, bwana, hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Kama hiyo ni kweli na unajua . . . Hiyo ni kweli? Naam, bwana.

¹⁹⁹ Sasa hivi hamwoni? Ni kitu gani? Ni ile Ishara ikitambulisha ya kwamba Yesu Kristo alifufuka toka katika wafu na ni yeye yule jana, leo, na hata milele, akitenda kazi kupitia mwili wa kibinadamu kama tu alivyofanya kule kabla ya Ibrahimu, lile Kanisa teule, kabla ya Sodoma. Naye Yesu alisema, “Jambo hilo litarudi tena, katika kuja Kwake Mwana wa Adamu.”

²⁰⁰ Hapa, huyu hapa mtu mwingine anayeketi hapa, akiniangalia moja kwa moja, mawasiliano halisi. Mtu huyo anaugua ugonjwa wa tumbo na ugonjwa wa mgongo. Jina lake ni Bw. Flannigan. Sikujui, bali hiyo ni kweli. Huyu ni mke wako anayeketi hapo karibu na wewe. Anaugua, pia. Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia sasa, na mawasiliano yako mazuri ya imani? Mke wako ana shida ya mgongo. Naye ana

shida ya ugonjwa wa wanawake, iko kwenye tumbo la uzazi. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI.

²⁰¹ Sasa, ni kitu gani? Ni nani anayefanya jambo hilo? Biblia ilisema, ya kwamba, “Yeye ni Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika hali yetu ya udhaifu.” Biblia ilisema, “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili,” katika kuhubiri Kwake, likitenganisha, wala halimjali mtu mashuhuri, wala madhehebu, wala chochote kile. Halafu tena hujitambulisha lenyewe kama nini? “Huyatambua mawazo yaliyoko moyoni.” Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli kabisa. Laiti tu ungaliamini hilo? Liamini tu kwa moyo wako wote.

²⁰² Kuna bibi anayeketi papa hapa. Yeye ana vivimbe. Hatoki hapa. Anatoka Sacramento. Jina Lake ni Bibi Bradley. Simama kwa miguu yako, kama hiyo ni kweli, mama, nasi hatufahamiani. Na uinue mikono yako kama hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Ninaamini kabisa vimeondoka. Sasa huyo alikuwa tu mwanamke anayeketi pale.

²⁰³ Huyu hapa mama anayeketi hapa nyuma kabisa. Amevaa kofia, kwa namna fulani ni kofia ya hudhurungi. Ina manyoya. Anavua miwani yake. Ameketi pale, akiomba. Alikuwa akiombea jambo fulani litukie. Ni kitu gani kinachomfanya mwanamke huyo kufanya hivyo? Mwanamke huyo ndiyo kwanza aponywe ugonjwa wa moyo. Anamwombea ndugu yake, naye ana ugonjwa wa moyo. Pia ana shemeji yake ambaye hajaokoka, na a—anamwombea apate kuokoka. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Kama hayo ni kweli, mama, simama kwa miguu yako, ili kwamba watu wapate kujua. Alikuwa ameketi moja kwa moja pale, akisema jambo hili, akiwaombea hao watu wakati huo. Kama hiyo ni kweli, pungu mkono wako, mama, huku na huko, wapate kuona.

²⁰⁴ Ningewezaje kumwambia kile alichokuwa akiomba, kutoka hapa jukwaani?

²⁰⁵ Huyu hapa mtu anayeketi papa hapa. Anaumwa magoti. Anamwombea rafiki ambaye ni kiwete. Yeye—yeye, kweli, hatoki hapa. Anatoka Santa Maria, mahali panapoitwa Santa Maria. Na jina lake, wanamwita Tony. Simama, kama hiyo ni kweli. Hatufahamiani.

²⁰⁶ Shikilia ishara yako mbele ya maombi yako! Mungu, wakati Malaika huyo wa Bwana alipokutana na mimi miaka mingi iliyopita... Wakati nilipokuja hapa kwa mara ya kwanza, niliwashika watu mkono, niliwaambia ninyi ya kwamba Yeye aliniambia jambo hili lingetimia. Sasa kuna jambo kubwa kuliko hilo. Unaona? Unaona? Na linaendelea daima, (kwa nini?) likishikilia hiyo Ishara mbele ya hilo. Unaona, Roho Mtakatifu, Mwenyewe, anaishi. Yeye ndiye anayefanya jambo hilo. Yeye alisema.

207 Sasa kama mtu yeyote ana tashwishi, wazungukie watu hawa na uaulize kama nilipata kuwaona, kuwajua, ama kitu kingine chochote kile. Wako hapa. Linaanza kutukia mahali pote jengoni sasa.

208 Sasa, hapa, kama Mungu anaweza kutambua jambo hilo, hebu niwaambieni jambo fulani. Kuna umati wa ninyi hapa, usiku wa leo, mnaohitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuishikilia ile Ishara. Mna-, mna-...Mnafikiria tu kwamba mnao, wakati hamnao. Msibahatishe, enyi marafiki. Niaminini. Kama mnaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu...Ama, samahani, sikumaanisha kusema jambo hilo. Sijiiti nabii. Mtumishi wa Mungu, kama mnaamini mimi ni mtumishi wa Mungu, ninawaambia, katika Jina la Bwana.

Tunapoinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu.

209 Huu ni ule wito mkuu. Ninamtaka kila mtu aliyepo hapa ndani, ambaye si Mkristo, aje hapa kwa dakika moja na hebu nipate kuomba pamoja nanyi, na kuweka mikono juu yenu, wakati Roho Mtakatifu akiwa yupo juu yangu, wakati upako ukiwa hapa. Ishara imeonyeshwa, shuhuda zisizokanushika! Mtanyamaza kimya kabisa? Ondokeni vitini mwenu na mje hapa sasa.

210 Kama dada huyo hapo, ama yeyote yule anayeongoza nyimbo, atupe sauti ya muziki sasa.

211 Tafadhali njoni. Na kila mtu tu asiye Mkristo, na aje hapa na asimame hapa madhabahuni, kwa muda kidogo tu. Hilo ni zuri. Bwana akubarki, ndugu yangu. Bwana akubariki, dada. Njoo moja kwa moja kuzunguka madhabahu hapa. Kila mtu...

Njoo, kila mtu aliyekandamizwa na dhambi,
Kwa Bwana kuna rehema.

212 Sasa je! mtafanya hivyo? Naam. Njoni hapa moja kwa moja, simameni hapa kwa dakika moja, ninyi msio na Kristo. Angalieni, muda umeenda mno, wapendwa. Malaika wa mauti huenda akatenganisha kati ya Bibi-arusi na kanisa, wakati wowote. Je! hamtaninii...

Kila mtu aliyekandamizwa na dhambi,
Kwa Bwana kuna rehema,

Je! msingependa kuja sasa wakati wakiimba?

Hakika atakupi raha.

213 Kwa nini? Anakupa ile Ishara, ndipo umepumzika, unaona. Una utambulisho, Bwana alituma Ujumbe Wake, akautambulisha, ile Nguzo ya Moto.

Mtumainini tu, ...tu

214 Enyi Wakristo, ninyi mlio na ile Ishara, ombeni. Enyi wenye dhambi msio na Kristo, mnaombwa mje, wakati Yeye

ametambulishwa kwa udhahiri sana hapa, kama ile Ishara. Ile Ishara, Yeye hajafa, amefufuka toka kwa wafu. Je! mtakuja sasa?

Atakuokoa, Atakuokoa sasa.

Mtumainini tu. . .

²¹⁵ Mtumainini tu! Unasema, “Ndugu Branham, sijui jinsi ya kufanya jambo hilo.” Njoo hapa, yote tu unayopaswa kufanya ni kusimama tu moja kwa moja. Msikilize Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo ambavyo vitu hivi hufanya kazi, msikilize yeye tu. Yeye aliliahidi. Kama tu vile alivyoahidi kufanya mambo haya katika siku ya mwisho, Yeye aliahidi kuwaokoa waliopotea.

²¹⁶ Unasema, “Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa, Ndugu Branham.” Hilo silo ninalokuuliza.

²¹⁷ Ninakuuliza sasa, “Je! umeokoka? Je! wewe ni Mkristo?” Kama sivyo, njoo huku. Njoo huku. Nakuomba, katika Jina la Kristo, njoo.

Mtumainini tu, . . .

²¹⁸ Ndiyo, ingieni moja kwa moja, njoni moja kwa moja madhabahuni sasa, ndugu.

Atakuokoa, atakuokoa,

Atakuokoa sasa.

Inakupasa kufanya nini?

Mtumainini tu, Mtumainini tu,

Mtumainini tu sasa;

Atakuokoa, atakuokoa

Atakuokoa sasa.

²¹⁹ Hiyo ni kweli, njoni moja kwa moja, wapendwa, njoni moja kwa moja. Kila Mkristo, omba sasa hivi. Kumbukeni, huenda watu wakaja, huenda hii ikawa ndiyo nafasi ya mwisho watakawahi kuwa nayo. Huenda hii ikawa. Kama anaweza kuyatambua mawazo ya moyo, Yeye ananiambia na ni kweli, “Wengi hapa ndani!” Usiache Shetani akudanganye, dada, ndugu. Usimwache yeye afanye jambo hilo, tafadhali usimwache afanye hivyo. Ipokee Ishara ya Mungu, usiku wa leo. Je! mtapenda kuja sasa? Sasa!

Mtumainini tu, mwamini tu,

Mtumainini tu sasa;

Atakuokoa, atakuokoa,

Atakuokoa sasa.

²²⁰ Ee Mungu, ninaomba hayo katika Jina la Yesu, ya kwamba utaangalia chini kwenye kusanyiko hili nawe utalichambua kabisa. Ninaomba ya kwamba Roho Mtakatifu aliye mkuu, ambaye yupo hapa sasa, yupo, akimwonyesha Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. . . Bwana, hakuna nafasi kwa Shetani kujaribu kusuguasugua kandokando yake. Wewe—Wewe uko hapa unajimbulisha Mwenyewe, umesimama

hapa katika mwili wa kibinadamu miongoni mwetu, na unajitambulisha kwa ile Ishara ambayo ingekutambulisha. Ile Ishara ni kwa ajili ya kumtambulisha Yesu Kristo, kufufuka Kwake. Nayo ndiyo hii hapa sasa ikimtambulisha Yeye, ikifanya yale yale aliyofanya wakati aliposimama hapa katika mwili wa nyama. Ee Baba Mungu, jalia watu waone na kutambua jinsi Maandiko haya yote na kadhalika yanatimilika kikamilifu.

²²¹ Jalia kila mtu aje sasa, Bwana. Nenda mara nyingine tena, Baba, na unene na mioyo, ili kwamba niwe na hakika ya kwamba... Nimekuomba, nami ninajua utafanya jambo hilo. Wewe daima hujajibu maombi yetu. Nena mara nyingine tena, Bwana. Nina hakika kuna wengine waliojisikia ya kwamba walipaswa kuja, bali hawakufanya hivyo kamwe. Wajalie, Bwana, ya kwamba watakuja sasa. Katika Jina la Yesu, naomba.

²²² Huku tumeinamisha vichwa vyetu, simameni (sivyo?) na hebu njoni sasa wakati tukiimba tena sasa. Basi njoni moja kwa moja huku, tokeni. Ninajisikia tu ndani ya moyo wangu; Hilo halikosei kamwe. Unaona?

Mtumainini tu,

²²³ Je! mtapenda kusimama? Njoni huku, simameni madhabahuni. Msininii... Huenda hii ikawa ndiyo nafasi ya mwisho utakayopata kuwa nayo. Kama swali hilo dogo limekuwa liko niani mwako, usi—usibahatishe hata kidogo. Usibahatishe, rafiki yangu. Unaona, mvua ilikuja, wala watu hawakujua hilo. Malaika wa mauti alipiga, watu hawakufikiri ndivyo ilivyokuwa. Musa aliwaambia itatukia. Yeye alithibitishwa dhahiri na Mungu.

²²⁴ Unasema, “Lakini mimi ni Mpresbiteri. Mimi ni Mmethodisti. Mimi ni Mbaptisti.” Sininii... Hilo hata halina uhusiano wowote. Unaona?

²²⁵ Njoni! Ninawaomba mje sasa, njoni na mumpokee kikwelikweli. Usininii... Ungekuwa na uhakika kabisa kama ulihakikisha tairi zako kabla hujaendesha gari mbio, chunguza gari lako kabla hujaenda kwenye likizo yako. Hivi hutapenda kupata kitambulisho cha ufufuo ndani yako? Je! ungependa kuja? Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Sita, saba, wanane zaidi wamekuja tangu wakati huo. Ninachukia sana kuufunga, namna hiyo. Je! utakuja? Mungu akubariki, ewe kijana. Akubariki, mama.

Sasa atakuokoa, atakuokoa.

²²⁶ Mungu akubarki, wewe kijana mwanamume. Kama unataka kujua, wewe ulikuwa ni mmoja wao. Ndiyo hivyo.

Mtumainini tu,

²²⁷ Sasa, hilo si ni jambo zuri, kuwaona wakija? Yeye... Unaona, Roho Mtakatifu kamwe hakosei. Yeye yuko sahihi kabisa.

Sasa atakuokoa, atakuokoa,
Atakuokoa sasa.

228 Je! una hakika kabisa sasa? Wakati muziki ukiendelea, tafadhali, polepole. Ungeweza kumwamini? Je! ungeweza tu kuamini Neno Lake?

229 Unasema, “Bwana, daima nimependa ule ushirika wa karibu, kitu hicho fulani halisi. Ninii, kwa kweli nautaka, Bwana, bali nimeona uigaji mwingi sana wa jambo Hilo.” Mbona, hakika, huyo ni Shetani, yeye—yeye hufanya hivyo kukutupa nje ya njia. “Ni—nimeona wale waliodai.” Hilo, hilo, unaona, linaonyesha tu kuna Lile lililo halisi mahali fulani. Kama ukipata dola ya bandia, ni kwa sababu tu imetengenezwa kutokana na kuigiza ile nzuri. Unaona? Unaona?

230 Kwani usije? Umtumaini kabisa kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Wakati Yeye ametambulishwa sana hapa mbele zenu, akijitambulisha hapa mbele ya karibu watu elfu tatu, akitokea. Amefanya hivyo hapo mbele ya watu elfu mia tano huko Bombay. Alifanya hivyo kabla, mbele ya watu watu mia moja na hamsini elfu ama elfu sabini na tano huko Durban, Afrika Kusini, ambako wenyeji wanaovaa mablanketi walipomjia Kristo kwa wakati mmoja. Unaona? Injili karibu inakwisha Marekani, wapendwa. Iko karibu kwisha. Kama mnaamini kwamba mimi nimefungamana na Mungu, kumbukeni, hiyo ni kweli. Je! mngependa kuja sasa?

231 Nitawaomba ndugu zetu wahudumu hapa, kama watatoka jukwaani, na kusimama kuzunguka mahali hapa, kujiunga na maombi haya ya kuwaombea watu.

232 Wengine wenu mnaweza kuinamisha vichwa vyenu, isipokuwa iwe mnataka kuja wakati wamesimama tu kuzunguka madhabahu hapa. Nitaomba pamoja nanyi.

233 Ninataka enyi watu mwende pale chini, kwa maana watu hawa watakuwa ni wafuasi wa makanisa yenu. Wamekuja, wakimkubali Kristo sasa.

234 Tafadhalini njoni, msimame hapa karibu, je! yupo mtu mwingine yeyote angetaka kuja wakati huu? Madhabahu ingali iko wazi. Huenda wasininii. . . Huenda ukawa umechelewa sana, punde si punde.

235 Wazia tu, Roho Mtakatifu mkuu akija, akimtambulisha Yesu Kristo kwamba yu hai, baada ya miaka elfu mbili, kuona tabia Yake hasa ikifanya jambo lile lile kama alivyoahidi litafanywa. Hiyo ni kweli.

236 Ninawashukuru sana, wapendwa. Ninyi mnaosimama hapa ndio wale wafanya kazi wa saa kumi na moja, ambao ndio wale kwanza mwingie. Nina furaha sana mlikuwa. Kila mmoja wenu, kumbukeni, Mungu ndiye aliyewaambia mje. Kibinadamu, msingefanya jambo hilo, bali Mungu aliwaambia kulifanya.

237 Sasa wakati ndugu hawa hapa wanaomba pamoja na mimi, Bwana na ajalie... [Mtu fulani anamwuliza Ndugu Branham kuhusu hao ndugu wahudumu wengine—Mh.] “Ati kama mhudumu yuko *hapa?*” Kabisa, ndugu wowote wahudumu, njoni hapa. Mna makanisa na kadhalika karibu na maeneo haya; njoni, kusanyikeni pamoja na watu hawa. Hawa ni watu ambao wamepotea, baadhi yao. Baadhi yao wanakuja kwa mara yao ya kwanza, nao wanasimama hapa sasa. Nendeni moja kwa moja miongoni mwao. Wakaribieni. Jichomekeni moja kwa moja ndani, muwaambie, “Mimi ni mchungaji *Fulani*. Niko hapa kuomba pamoja nawe, ndugu. Ninakupenda. Ninakupenda, nami niko hapa kuomba pamoja nawe.”

238 Angalia, njoni, baadhi yenu, njoni *huku*. Njoni huku, kuna nafasi hapa ndani. Baadhi yenu upande *huu*. Ninii tu. . .

239 Namna hiyo, ingieni moja kwa moja miongoni mwa watu, useme, “Mimi ni mchungaji *Fulani wa fulani*.” Weka mkono wako juu ya bega la mtu fulani, useme, “Ninakuja kuomba pamoja nawe, dada mpendwa, ndugu mpendwa. Nimekuja kukusaidia uende kwa Kristo.” Ingia moja kwa moja ndani sasa, useme, “Mimi, nitafurahi kukufanyia jambo lolote niwezalo. Tutaomba sasa.”

240 Nimeliomba kusanyiko hili kama watainamisha vichwa vyao pamoja nasi sasa, wakati tukiingia katika maombi.

241 Kila mmoja wenu ninyi wachungaji, mchukue mtu, mchukue mtu uliyemwekea mikono. Kila mchungaji, ingieni miongoni mwa watu, ili kwamba upate kuweka mikono yako juu ya mtu fulani. Namna hiyo.

242 Kila mmoja wenu akiri ya kwamba alikuwa makosani. Na, kumbukeni, Yesu yeye yule basi yupo papa hapa sasa. Kwa hiyo nisaidie, ile Nuru iko papa hapa miongoni mwenu. Yeye ni Kristo. Mwombe tu akusamehe, na Mungu atakusafisha na kila dhambi. Kaa tu papo hapo sasa. Na mchungaji atakuongoza moja kwa moja kwenye toba na moja kwa moja kwenye ile Ishara, na hili litamaliza jambo hilo.

243 Bwana Yesu, tunakuletea, usiku wa leo, Bwana, lesa hizi zote na kadhalika, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, kwamba utamponya kila mmoja wao, kwa ajili ya utukufu Wako.

244 Baba, wasikilizaji hawa, tunakuona wewe umejitambulisha dhahiri sana kwa Neno Lako. Umejitambulisha kama Utu wa Bwana Yesu, hapa katika namna ya Roho Mtakatifu, ukitenda kazi miongoni mwa watu, ukiyatambua mawazo yaliyo moyoni mwao, ukiponya magonjwa yao, na ukiwaita watubu, Mwana mkuu na mwenye nguvu wa Mungu. Ninawatoa Kwako, Baba, kama ishara ya imani yao katika ninii Lako lililoaminiwa. . . katika Neno Lako lililobashiriwa. Neno ulilosema ya kwamba utalininii. Ninaamini, Bwana, ya kwamba utawathibitishia Hilo. Wao ni Wako. Wao ni tunu za upendo; ninawatoa Kwako, Baba.

Katika Jina la Yesu Kristo, mwokoe kila mmoja wao, Bwana. Jaza kila mmoja wao na Roho Mtakatifu. Tujalie hilo, Ee Mungu wa Milele. Jalia Roho Wako na rehema ziwe juu yao, kwa ajili ya utukufu Wako.



ILE ISHARA SWA64-0208

(The Token)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 8 Februari, 1964, katika Uwanja wa Maonyesho wa Wilaya ya Kern, huko Bakersfield, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2008 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org